

KUSIMAMA KATIKA PENGO



Asante, Ndugu Neville. Tuendeleo kusimama kwa muda sasa, tunapoviinamisha vichwa vyetu kwa maombi. Hebu tunamisho vichwa vyetu. Na kama kuna ombi maalum, hebu na lijulikane kwa mikono yenu iliyoinuliwa juu. Sasa shikilia moyoni mwako mambo yale ambayo unahitaji, na muombe Baba wa Mbinguni apate kukukirimia.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako sasa katika Jina la Bwana Yesu. Tunakuja, tukiadini kwamba mambo yale tunayoyahitaji yabidi yajulikane katika maombi. Na kama tungeadini kwamba tunapokea tunachoomba, kingekirimiwa. Sasa ahadi hiyo ni kweli kabisa. Miaka yote hii, tumeona Hilo likijaribiwa, nasi tunajua kwamba Hilo ni kweli. Tunataka kukushukuru Wewe, kwanza, kwa kuhifadhi maisha yetu na kuturuhusu sisi kurudi hapa tena, pamoja, tukiwa tumekusanyika hapa katika kusanyiko la Bwana.

³ Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili na kwa ajili ya mchungaji, na kwa Ukweli mkuu ambamo limejengewa hapa na linasimamia. Tunakushukuru Wewe kwa kila mtu ambaye yuko katika Uwepo wa Kiungu. Nasi tunaomba kwamba Wewe utaturehemu, leo, na utujalie ufahamu ambao tunahitaji, ili kwamba tuweze kuwa watumishi hodari kwa ajili Yako. Ni hamu ya mioyo yetu kukutumikia Wewe kwa kicho na kwa moyo wa kweli, na kwamba uweze kupata yaliyo bora sana katika maisha yetu. Kila siku, hebu mienendo yetu iwe hivi kwamba Wewe utapendezwa na mambo tuliyotenda kwa ajili ya siku ile.

⁴ Sasa tunaomba kwa ajili ya wagonjwa wote na wahitaji, leo, ambao wako kwenye Uwepo wa Kiungu hapa, na mbele ya madhabahu Yako kila mahali ulimwenguni, ili kwamba yule Yehova mkuu atakuja katika uwezo Wake na kuponya wagonjwa wote na wanaoteseka. Jipatie utukufu kwa Jina Lako Kuu! Bariki kila siri iliyo moyoni, asubuhi hii, ya hizo haja za maombi. Tunaomba, sasa, Wewe unapotazama katika kila moyo, na kuona walilotaka walipoinua mikono yao, na uwape haja zao. Na utubariki tunapoundelea kukuabudu Wewe. Na tunapotoka kwenye Jengo hili asubuhi hii na kurejea makwetu, na tuweze kusema kama wale ambao walikuja kutoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo Yeye aliponena nasi njiani?” Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

⁵ Ngingependa kusema kwamba ni vizuri, asubuhi hii, kuwepo hapa tena katika kusanyiko la watu, katika Uwepo wa Bwana. Na ni miezi michache tangu niliporudi. Na Jumapili iliyopita nilikusudia kuja humu, bali na—nadhani haikuwa mapenzi ya

Bwana. Kwa namna fulani, hili bonde hapa sio mahali pazuri kwa afya yangu. Mara nijapo kwenye bonde hili, ninapatwa na maradhi kwa ajili ya hewa ya hapa, ndipo ninashikwa na marugurugu mwili mzima. Nami nafikiri hayo marugurugu yalisambaa hadi tumboni, nami nikawa mgonjwa sana, ni... kutetemeka, na kudhoofika, na baridi. Basi sikuweza kuja humu, ingawa niliinuka na kujaribu kujilazimisha kufanya hivyo. Basi na—najua kwamba ni—nime... Bonde hili lina afya mbaya sana, na lina afya mbaya na—na sipaswi kuishi humo.

⁶ Sasa tunataka kutoa taarifa, tumekuwa na wakati mzuri sana katika utumishi wa Bwana, nje kule katika sehemu mbalimbali za nchi ambako Bwana ametuita kuhudumu. Basi sasa sikutarajia kuzungumza asubuhi hii juu ya jambo fulani hasa, hata hivyo Ndugu Neville alinitaka sana ku—kusema kitu cha kuwepo hapa na watu. Kwa hiyo mimi... Yeye sikuzote ana hisani katika mambo hayo, jinsi sote tumjuavyo Ndugu Neville. Nasi tunampenda Ndugu Neville. Sasa, hakuna siku ambapo simuwazii yeye na mkewe na jamaa, na watoto wake, kuwaombea. Mungu na ampe nguvu za kuendelea, kusonga mbele! Kama tujuavyo, muda wetu unakwisha. Tumekaribia sana... ya kesho, ambayo ni Nuru za jioni za leo. Na mimi...

⁷ Jamaa yetu iko upande wa Magharibi. Sote tulifanikiwa. Nami niliongezeka ratili kumi na mbili, ila nimepoteza kumi ya hizo tangu niliporudi. Na Billy Paul aliongezeka ratili kumi na nane. Na Rebekah, na Sarah, na Joseph, wote wameongezeka. Kama kawaida, mke wangu hakuongezeka. Kwa hiyo—kwa hiyo nisingethubutu kusema hilo juu hapa, unajua, sababu lazima niende nyumbani baada ya muda mfupi. Kwa hiyo mimi... Bali tulikuwa na wakati m—mzuri, mzuri sana, na nimeshukuru sana. Sisi...

⁸ Ni vibaya kwa namna fulani, nilifikiri, kurudi, lakini kuna jambo moja kuu, mambo mawili hasa tuliyokosa, kwamba hakuna mahali pengine panapoweza kuchukua mahali pake. Jambo moja, marafiki wetu hapa, na kanisa. Haidhuru twende wapi, tunapata marafiki, nasi tunashukuru kwa ajili ya marafiki wetu. Lakini kuna jambo fulani kuhusu rafiki wale ambao wameambatana nawe katika hali na shari, kwamba hakuna njia ya kuwabadilisha hao marafiki. Haidhuru marafiki wengine wawe nini, hakuna njia ya kubadilisha rafiki kama huyo. Unashikamanishwa tu nao, ninyi ni mmoja. Na sisi, pamoja, tukitazamia Kuja kwa Bwana, siku zinaposonga mbele. Na ni vigumu kwa namna fulani kujaribu kufikiri kwamba mngeweza... Hamwezi kutenganishwa.

⁹ Inanikumbusha Andiko moja ambalo naamini Paulo aliandika, akasema katika Wakorintho, kwamba, “Wala yaliopo, wala yajayo, na hakuna mamlaka, wala uchi, njaa, adha, au kiumbe cho chote kilichopo, wala uzima, wala mauti, vinaweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu.”

Jinsi ambavyo hata mauti yenyewe hayatatutenganisha kamwe, kwa sababu tumekwisha unganishwa pamoja moyoni, katika ushirika huu mkuu katika Neno la Mungu. Na hata mauti yenyewe, hayatatutenganisha. Tutaunganishwa katika Milele kuu, kwa majira yote na nyakati zote.

¹⁰ Na kwa hiyo watoto . . . Asubuhi, tungeenda kanisani, bila shaka. Bali kila mahali unapokwenda, hakuna hata . . . Si yale Maskani madogo kule pembeni. Na kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo. Mimi—natamani kusikia kengele ile ndogo ya kale na mimi . . . ikilia pale juu, asubuhi. Na nadhani hailii wakati huu, kwa sababu bado hawajaweka mnara bado, kwa ajili ya kengele.

¹¹ Na halafu kukusanyika hapa kwenye Barabara ya Nane na Penn, ambapo yapata miaka thelathini na mitano iliyopita, nikipiga magoti hapa kwenye bwawa la zamani, kujenga kanisa langu la kwanza, na jinsi Bwana Yesu alivyoshughulika nami katika jambo hilo. Na leo hii linasimama kama madhabahu madogo hapa. Na tofali na chokaa, linasimama kama madhabahu. Bali mle ndani moyoni mwangu, ni madhabahu ambayo itadumu maadamu nina ufahamu. Ni . . .

¹² Na kinachofanya kanisa si jengo, ni watu ambao hukusanyika chini yake kumwabudu Mungu. Tunashukuru kwa mambo haya.

¹³ Na sasa nilifikiri, labda kwa kuwa muda wetu umeisha, karibuni, na—na hatuna muda mwingi uliobaki. Ningewasimulia kwa kifupi mambo fulani yaliyotukia. Ndiposa nitanasa kanda wakati nipo hapa, kwa sababu niliwaahidi ninyi nyote, unaona, kwamba ujumbe wo wote mpya, ujumbe wa kanda, utatoka kwanza kwenye jukwaa hili. Hapa ndipo ambapo kanda zote zinaponasiwa, sio nje huko. Sasa, Ndugu Jim na hao wengine huenda na kuuza kanda kwenye mikutano, na kadhalika. Bali huko sikuzote ni juu ya kitu ambacho kimetoka hapa kwanza. Unaona? Hebu chunguza kila mahali po pote kule nyuma, utaona jambo hilo. Hiyo ni ahadi yangu kwenu, na itaendelea jinsi hiyo mpaka Bwana Mungu alibadili.

¹⁴ Basi ninafikiri sasa kwamba wanunuzi wetu wa kanda, ambao wako duniani kote, Ujumbe unaotoka hapa, huizunguka dunia. Unaona? Kule nje misituni na kila mahali, Huo huenda kwa kanda zilizonaswa. Na kwa makafiri na kadhalika, hufasiriwa katika lugha nyingi, nyingi sana mbalimbali. Kwa hiyo ninataka, wakati nipo hapa, Bwana akipenda, kunasa kanda mpya. Na labda, kama mchungaji hana kitu kinachomwasha moyoni mwake usiku wa leo, vema, ningetaka labda kunasa kanda usiku wa leo.

¹⁵ Nami basi ninakwenda Arkansas kesho, na, au Jumanne, hasa, Jumanne asubuhi, kusaidia katika mkutano mdogo kule pamoja na Undugu wa Wakristo Duniani. Nafikiri . . . Au pengine nilitamka vibaya hilo. Ni kitu kuhusu Undugu wa

Wakristo Taifani. Kwa kweli sijui. Ninasikitika. Hilo ni baya sana, sivyo? [Ndugu fulani anasema, “Shirika la Undugu wa Kikristo.”—Mh.] Asante, bwana. Shirika la Undugu wa Kikristo. Nami nilitarajiwa kuhubiri, tangu Jumapili hii, na kuendelea. Bali nimetenga siku ya leo kwa ajili ya Maskani, nipate kuwemo humu. Na halafu—halafu nitatoka Ijumaa . . . Hiyo ndiyo, bwana, ni . . . Ijumaa ndipo ambapo hiyo—hiyo mikutano itamalizika kule. Nami nitajaribu kurudi Jumamosi usiku, kusudi niwe hapa Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, nitanasa kanda nyingine. Na pengine wakati mwingine, kuanzia sasa, nataka kunasa kanda chache kabla hatujaondoka.

¹⁶ Na basi kwa kweli ninakazana kwenda Baton Rouge, Louisiana, kwenye mkutano ule. Halafu—kisha nitarudi. Baadaye ninatakiwa kwenda, kwa hali zo zote, kule Anchorage. Unaona? Na—na kutoka Fairbanks na Anchorage, kwa Wakristo Wafanyi Biashara wa Injili Yote, kwenye mikutano ile. Ndipo nitarudi. Na kama Bwana akipenda, hadi Chicago katika juma la mwisho la Julai.

¹⁷ Ndipo nadhani basi, mnamo wakati huo, itanibidi kuwapeleka watoto upesi kwenda Arizona tena waende katika . . . kuwapeleka huko shuleni. Kwa sababu, Charlie, yanibidi kuwepo hapo mnamo Agosti kumi na tano. Kwa hiyo na—nataka kuwa nimerudi wakati huo, Bwana akipenda, kule Kentucky. Kila mtu anacheka, pengine baadhi ya wageni wasingepua hilo lilimaanisha nini. Na kwa namna fulani tu natumaini halionekani ni baya toka jukwaani, lakini hapo ndipo majira ya kindi yanapotimia. Kwa hiyo, Mama Cox, ninategemea jambo hilo, unaona, ili nipate majuma machache chini kule ya likizo yangu.

¹⁸ Sasa, ninaamini ile. . . Nina kitu fulani hapa ambacho Billy aliniandikia, maandishi machache. Na moja ya hayo yanasema, “Baba, Ndugu Neville anataka kujua kama ungeweza kuwaweka watoto wawili wakfu.” Hakika, hilo ni sawa. Pia, naam, tuna i—ibada ya kuwaweka wakfu ambayo. . . Ni heri basi tuifanye hiyo sasa hivi. Pia nafikiri kwa namna fulani tutachukua dakika arobaini na tano zijazo, au kitu kama hicho, katika kuelezea kifupi juu ya baadhi ya mambo ambayo yametukia.

¹⁹ Sasa, watu wengi na makanisa, kwa kuwa wakati mimi. . . Hii ni Maskani ya watu wote. Haijawa madhehebu kamwe, na Mungu ajalie kwamba isiwe, isiwe kamwe. Kwa sababu, tunapenda mahali hapa ambapo hatuna—hatuna sheria ila upendo, hatuna kanuni ya imani ila Kristo, hatuna kitabu ila Biblia. Pia, hatuna uanachama, tuna ushirika sisi kwa sisi, kwa watu wote, madhehebu yote. Kila mtu amekaribishwa na tuna—tunashiriki Neno la Mungu, mahali ambapo kila mtu anaweza kujisikia amekaribishwa iwezekanavyo. Basi jambo muhimu, tunampenda Bwana Yesu sana. Na—na sisi si kundi lenye—lenye elimu hapa. Sisi ni watu wa kawaida tu ambao wanajaribu

kuisoma Biblia na kutoweka tafsiri yo yote Kwake nje ya yale isemayo. Ni. . .

²⁰ Naamini kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja kwa Biblia. Sasa, iwapo wao. . . Yeye atauhukumu ulimwengu. Na iwapo hakuna kanuni ya kuhukumia, watu watajuaje la kutenda? Unaona? Ingekuwa Mungu. . . Usingeweza ku—kumshtakia Mungu dhuluma. Na Mungu yambidi awe na kitu fulani kama kanuni Yake, anachowahukumia watu kwake. Kwa hiyo, Yeye akiuhukumu kwa kanisa Katoliki la Kirumi, basi kanisa la Kiyunani, kanisa Katoliki la Kiothodoksi, na mengi ya hayo, hakika yamepotea, na ulimwengu wote mwingine wote. Kama akiuhukumu kwa kanisa Katoliki la Kiothodoksi ya Kiyunani, na siyo kwa kanisa la Kirumi, basi mengine. . . Basi kanisa la Kirumi na mengine yote yamepotea. Kama Yeye akiuhukumu kwa kanisa la Kiluteri, basi Wapresbeteri wamepotea. Akiuhukumu kwa Wapresbeteri, Waluteri na Wabatisti wamepotea. Unaona? Kwa hiyo kama akiuhukumu kwa Wapentekoste, basi wote wasio Wapentekoste wamepotea.

²¹ Lakini Yeye hatauhukumu kwa kanisa lo lote, nionavyo mimi, kwa sababu kuna tofauti nyingi sana na fujo nyingi mno. Bali Yeye atauhukumu, Biblia inasema, “Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo.” Sasa, hayo ni Maandiko. Sasa. . . Na Biblia ilisema, kwamba, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa hiyo, Yeye ni Neno, nalo *Hili* ni Kristo katika hali ya andiko. Na katika kitabu cha Apokalipso kwa Wakatoliki; Ufunuo kwa Waprotestanti, katika sura ya 22 hapo Kitabu hiki kilipomalizika, Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, “Mtu ye yote akiondoa Neno moja toka kwenye Kitabu hiki, au kuongeza neno moja Kwake; huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima.” Kwa hiyo mimi. . . Sababu ya sisi kuamini hili, na kudumu vile vile hasa. Hakuna kitu. . . Yeye anaweza kutenda mambo ambayo Yeye hakuyaandika humu, tunajua hilo. Bali maadamu tunadumu na yale ameandika, hilo ni sawa.

²² Na sasa, katika kuwaweka watoto wakfu, watu wengi, Wamethodisti huwanyunyizia. Na—na nafikiri hupokea ushirika wao wa kwanza katika kanisa la Kikatoliki, au la Kiluteri, kwenye umri wa miaka kumi na miwili, na namna fulani ya i—ibada ya ubatizo wanapozaliwa. Na—nafikiri watoto wananyunyiziwa. Na—nafikiri kwamba jambo hilo liliwatoa Wanazarayo kutoka katika Methodisti, miaka mingi iliyopita, katika ubatizo wa watoto. Nadhani hilo ni kweli, Ndugu Brown. Na—na—naamini kwamba hilo ndilo lilivunja kanisa la Kimethodisti na la Kinazarayo, sababu Wanazarayo hawakukubali ubatizo wa watoto. Bali kwetu sisi, hapa kwenye

Maskani, kama tutadumu na yale Biblia isemayo, hakuna mahali katika Biblia ambapo waliwahi kumnyunyizia mtu ye yote, licha ya mtoto mchanga, sembuse mtu mzima. Bali wao...Biblia inasema, mahali pekee pa Biblia yetu kwa watoto, “Wakawaleta watoto wadogo kwa Yesu, Naye...apate kuwawekea mikono Yake na kuwabariki.” Naye akasema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwakataze, kwa maana watoto kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.”

²³ Sasa, kwa hiyo, tunajua kwamba tu mikono dhaifu, mimi pamoja na mchungaji, au mchungaji ye yote, kuchukua mikono ya Bwana Yesu. Na kama Yeye angekuwa hapa asubuhi hii, hawa wazazi wangelimleta mtoto huyo kwa Kristo. Bali kwa kuwa tupo hapa tukimwakilisha Yeye, kwamba tunamwakilisha Yeye, wao wanawaleta watoto kwetu. Nasi tunawawekea wakfu kwa Bwana, kwa kuweka mikono yetu juu yao, kwa ukumbusho wa Neno Lake kuu pamoja na tendo Lake. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyowawekea wakfu watoto wadogo.

²⁴ Nilifikiria pengine mama fulani anaweza awepo hapa na mtoto wake, ambaye hajawahi kuwekwa wakfu kwa Bwana, kwamba angetaka kuja pamoja na mama hawa au baba ambao watawawekea wakfu watoto wao. Twawaleta tu juu hapa na kuwatoa kwa Mungu, na kuwaombea, na kumwambia Bwana kwamba tunawawekea mikono, kana kwamba ni badala Yake. Na jambo hilo linaafikiana na Maandiko kuliko yote niliyowahi kuona. Sasa, unaweza ukachukue kitabu chako na kuona jambo fulani ambalo kundi fulani la watu lilisema, bali ninamaanisha ambalo Neno lilisema, unaona. Basi nafikiri nimelifanya dhahiri sana, sana.

²⁵ Sasa kama mpiga piano (Wewe ndiye mpiga piano, ndugu?) atakuja hapa. Je! si ni vibaya sana, katika kanisa langu mwenyewe, kuuliza, “Mpiga piano ni nani?” Karibuni nipige hodi mlangoni. Sawa. Wanaimba wimbo huu mdogo, au kuucheza.

Waleteni, waleteni,
Waleteni watoto wachanga kwa Yesu.

²⁶ Na wakati kusanyiko linauimba huu, hebu na tusimame kwa miguu yetu. Hebu mama na baba ambao wanawaleta watoto wao wachanga, waje sasa wasimame. Sawa.

Waleteni, waleteni,
Waleteni watoto wachanga kwa Yesu.

Sasa, mchungaji...Sasa tuna jamaa—jamaa mdogo hapa amelala. Na wakati mwingine wao huitikia “amina” kwa sauti kubwa zaidi, kwa hiyo tunaelewa hilo, wao ni watoto wachanga. Jina lako ni nani, bwana? William Henry Vincent. Na msichana wako mdogo? Christina Maria Vincent. Ni jamaa mdogo anayependeza jinsi gani anayelala kwenye—bega la baba yake. Nimchukue? Christina, siwezi kuchukua mahali pa baba

yako hapa, unaona. Hebu . . . Tafadhali weka mikono yako juu ya mtoto.

Tuinamishe vichwa vyetu.

Baba, yetu wa Mbinguni, tunakaribia Kiti Chako cha Enzi, kwamba leo, huko ng'ambo, imani yetu inatuinua kupita mwezi, nyota, kupita mfumo wa jua, katika Uwepo wa Mwenyezi. Tunamleta huyu mtoto mdogo apendezaye. Hatujui tunachoshikilia katika mikono yetu, Bwana. Inaweza iwe mtumishi maarufu Kwako, katika siku zijazo. Twatumaini kwamba ndivyo ilivyo. Lakini baba wa mtoto huyu amemleta mtoto huyu kwetu, ili tumwekee mikono. Kwamba, tumeungama kuwa watumishi Wako kufanya kazi badala Yako hata utakaporudi, hapo Wewe utachukua mambo yote. Hadi wakati huo, Bwana, yatubidi kukutumikia Wewe kwa ukweli na uaminifu.

Na huku mikono yetu ikiwekwa juu ya msichana huyu mdogo, tunambariki katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Naamini kwamba Wewe utampa yeye maisha marefu, kama Yesu akikawia, na awe mtumishi mkuu Kwako Wewe. Bariki nyumba ambamo atalelewa. Hebu na akuzwe katika maonyo ya Mungu, na kumtumikia Yeye siku zote za maisha yake. Wabariki wazazi wake, na waishi kumwona huyu mtoto akiwa chombo cha kuheshimika kwa Bwana, kwa sababu ya kitendo chao leo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Miaka thelathini iliyopita, nikisimama katika mlango wa shule hapa kwenye Utica Pike, je, niliwahi kujua kwamba yule mvulana mdogo, sisi, wenye soni, tulitazamana, kwamba siku moja ningemwekea mikono mjukuu wake, kumweka wakfu kwa Bwana Mungu wa Mbinguni. Mpokee mtoto John asubuhi hii, Bwana, kama mtumishi Wako. Mama na baba kwa ushujaa wanamleta, kumrudishia Mungu ambacho kimetolewa kwao wakakitunze. Na waishi maisha yenye afya na ya nguvu, na ushupavu, katika Kristo. Sasa tunakupa Wewe mtoto huyu mdogo, katika Jina Lake Yesu Kristo, kama maisha ya utumishi. Na aishi maisha marefu, kukutumikia Wewe.

Msichana mdogo amewekwa wakfu? Jina lake ni nani? Karla.

Vile vile, juu ya mtoto Karla, tunaweka mikono yetu, asubuhi hii, na kumweka wakfu kwa utumishi wa Yesu Kristo. Mungu, mbariki. Jalia aishi maisha marefu, yenye furaha. Na awe mtumishi Kwako, sikuzote za maisha haya. Lijalie, Bwana. Bariki nyumba yake. Ijalie na iwe siku zote mahali pa maombi na imani. Ninakupa Wewe huyu msichana mdogo apendezaye, asubuhi hii, toka kwenye mioyo ya baba na mama wanaosimama kwenye madhabahu haya madogo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Babaye anasema, “Jina lake ni James Pool.”—Mh.] Mvulana mdogo. Amechukua jina la Jim, [“Ndiyo.”]

Baba yetu wa Mbinguni, baba wa hawa watoto wadogo anashikilia sasa mkononi mwake hazina ya mwisho ambayo Wewe umempa katika namna ya mtoto, akachukua jina la baba yake, James. Mungu, jalia kwamba atakuwa mtu wa hekima kama Yakobo na katika Biblia. Naomba kwamba Wewe utampa maisha marefu yenye afya, Bwana. Na ainuke, na kama kuna ya kesho, mjalie alichuke Neno la Mungu. Lijalie, Baba. Kwa ukumbusho wa yale Yesu Kristo Bwana wetu aliyafanya Yeye alipokuwa duniani, naweka mikono yangu juu ya mtoto James Pool na kumweka wakfu kwa huduma ya Mungu. Katika Jina Lake Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, James! Mbariki Mtoto huyu!

Mvulana mdogo; wawili wao sasa. Wasemaje? Jerry Dean Allen.

Bwana Mungu, juu ya kichwa cha mvulana huyu mdogo, Jerry Dean Allen, baraka za Yesu Kristo na zikae. Tunapomwekea mikono yetu, tunapoyaweka wakfu maisha haya machanga Kwako. Bariki nyumbani kwake, wazazi wake. Na aishi maisha marefu ya furaha na ya utumishi kwa Mungu wetu na Mungu wake, Ambaye tunamtoa Kwake sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, ewe mtoto!

²⁷ Sasa, nafikiri hiyo ni kama—kama hayo yamekwisha sasa. Sasa tumewahi sawasawa kwenye wakati, kwenye saa tano. Sasa, unajua, naweza kuwazia tu, nikiwaona hao akina mama wakija, na akina baba, pamoja na hao watoto wachanga. Ningeweza kuwazia kuhusu Yusufu na Mariamu, asubuhi ile ya kuwekwa wakfu kwa Bwana Yesu.

²⁸ Ndugu Kidd, nilikuwa nikihojiana na mtu fulani afisini, lakini ni—nilisikia furaha yako asubuhi hii nje hapa, wa—wa mtu wa umri wako. Nami nafikiri ulikuwa unasimulia kuhusu jinsi Bwana alivyokuponya ukiwa kwenye . . . kwenye maktutano. Na karibu niharibu gari langu, asubuhi moja, kumfikia yule mzee . . . Yeye ni mhudumu wa siku nyingi.

²⁹ Hebu fikiria, mtu huyu alikuwa, maskini mkewe yuko hapa, alikuwa anahubiri Injili kabla ya mimi kuzaliwa. Akihubiri Injili hii, kule juu kwenye milima na mabonde ya Kentucky na Tennessee, na wachimba makaa, huku anafukuzwa. Na wanaishi bila chakula. Na maskini mke wake hapa, akifua kwenye ubao wa kufulia, kwa yapata senti ishirini au thelathini kwa siku, ili kumpeleka mumewe uwanjani akahubiri Injili. Hili latosha kumfanya mtu asisimke, siyo?

³⁰ Na halafu kufikiria, kwamba huyu hapo amelala, wakati madaktari walio bora sana walisema, “Anakufa. Amezimia roho

yake, amejaa kansa ya kibofu. Hawezi kuishi ila masaa kadhaa tu, na hasa sana siku moja ama mbili.” Na hiyo imekuwa kama miaka miwili mitatu iliyopita, miaka mitatu iliyopita. Huyu hapa basi, asubuhi hii, mwenye afya, mzima, akimpa Mungu utukufu. Basi, ulikuwa na umri gani ulipoponywa, Ndugu Kidd? Ulikuwa kama umri gani wakati Mungu... Una umri gani, ana umri gani sasa? [Dada fulani anasema, “Themanini na miwili, thamanini na mitatu mnamo Agosti.”—Mh.] Themanini? Sawa. Alikuwa na yapata umri wa miaka themanini Mungu alipomponya. Basi je, Mungu anatushughulikia sisi wazee? Hakika, Yeye anatushughulikia. Ndiyo, bwana!

³¹ Alimponya Ibrahimu wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, na Sara alipokuwa tisini. Nao wakamzaa Ishmaeli, au samahani, Isaka. Sivyo? Tunafurahi sana kwa ajili ya jambo hili.

³² Saa mu wazuri sana, ningeweza kuzungumza nanyi asubuhi yote namna hii tu. Bali hebu na tusome sehemu ya Neno la thamani ndipo tuingilie ibada. Sasa, nadhani, kama ni mapenzi ya Mungu, ningependa kwa namna fulani niwaeleze kwa kifupi juu ya mambo yaliyotukia. Halafu usiku wa leo, kama Bwana akipenda, nataka kuzungumzia juu ya so—somo. Nataka kulinasa kwenye kanda, hasa, lipate kusambazwa. Ni... Na kama unataka kuja kusikiliza, sawa. Baada ya mchungaji kumaliza ujumbe wake, ndipo nitapata... Nitanasa kanda hii. Nataka kuhubiri juu ya *Kimulimuli Chekundu Cha Kuja Kwake*. Jinsi ambavyo kimoja cha vimulimuli hivyo kipo nasi sasa hivi! Na nataka kuzungumza juu ya hilo usiku wa leo, kimulimuli Chake chekundu. Yeye yupo hapa, akiwa karibu sana sasa hivi. Ile—ile Selo imeshushwa, gari la moshi limewasili.

³³ Hesabu, sura ya 16, kwenu ninyi ambao mtaifungua na kusoma. Hili ni Neno la Milele, kwa hiyo hebu na tulisome kwa kicho. Nataka kusoma aya mbili za Hesabu 16, aya ya 3 na ya 4, kupata msingi mdogo juu ya yale ninayotaka kusema.

³⁴ Na sasa, iwapo kanda hazikufunguliwa, ningomba wazifungulie sasa. Au kuziweka ili kwamba sehemu hii hapa itaweza kutumwa nje. Hii inakwenda nje. Kama mkitaka, mnaweza kuandaa kanda zenu ndani hapo ambapo sehemu hii hapa itatengwa na sehemu iliyobakia ya ibada? Unaona, hiki ni ki—kitu kipya. Sasa, kama mnaweza kuizua papa hapa, au lo lote mtendalo, vema, basi tuta... Mngetaka niikate kwa nukta moja, halafu niifungulie, ili iwape nafasi kujua mtaanzia wapi, au mnaweza kuanza hapo kwa vyo vyote? Kuanza kwa vyo vyote? Vema. Hilo ni sawa.

³⁵ Sasa tutasoma Hesabu 16:3 na 4.

Nao wakakusanyika kinyume cha Musa na Haruni, na kuwaambia, Ninyi inawatosha, kwa kuwa mkutano wote ni mtakatifu, kila mmoja miongoni mwao, BWANA

naye yu kati yao; nini basi kujitukiza juu ya mkutano wa BWANA?

Musa aliposikia maneno haya, akapomoka kifudifudi:

³⁶ Baba yetu wa Mbinguni, bariki Maneno haya machache. “Mawazo ya mioyo yetu, na matunda ya vinywa vyetu, yapate kibali mbele Zako.” Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

³⁷ Nataka ku—kuchukua hili kama kifungu, kwa yale ninayotaka kusema asubuhi hii: *Kusimama Katika Pengo*.

³⁸ Kuhusu wakati huu ambao tunazungumzia, au kusoma, bila shaka, sote tunaielewa kwamba ilikuwa hapo Dathani na—na—na Kora walikuwa wameamua kwamba—kwamba wangeingilia a—agizo ambalo Mungu alimpa Musa, wakisema, “Yakubidi kuuruhusu mkutano wote kufanya *kadha na kadha*. Wote ni watakatifu.” Na Mungu alikuwa amemwagiza Musa kuwaongoza watu hadi nchi ya ahadi. Nao wakasema, “Umejitalia madaraka mengi mno wewe. Wewe, ukijaribu kujifanya mtu wa pekee katika kundi hili ambaye—ambaye ana mamlaka yote.”

³⁹ Na hili lilimuudhi Mungu sana mpaka Yeye akamwambia Musa, “Jitenge ukaonduke miongoni mwao. Ni—nami nita—nitaliva tu kundi hilo lote, na kuanza kizazi kipya kwako.” Basi Musa akaanguka mbele za Mungu akasema Yeye itambi⁴⁰ aje juu yake. Unaona?

⁴⁰ Sasa, leo, kama Mungu angeamua kuwaangamiza watu, na kuna wakati ambapo Mungu alikuwa amechoka na kucheza zetu, daima tunakosea, ni nani angesimama kama Musa, leo, kwa ajili ya watu? Tungempata mtu wapi ambaye angesimama, au angeweza kusimama, kwamba Mungu angemkubali kama Yeye alivyomkubali Musa? Na maisha ya Musa mwenyewe duniani yalikuwa muhimu sana kwa Mungu mpaka yakazuia hasira ya Mungu, na Mungu asingemkiuka Musa. Hilo sikuzote lilikuwa tatizo kwangu mpaka mimi. . . Siku moja, katika ufunuo wa Maandiko, wazo hili lilinijia. Kwamba, unaona, Musa, katika kutekeleza, alikuwa badilisho kwa kila njia. Yeye alikuwa mfano wa Yesu Kristo.

⁴¹ Na wakati Mungu alikuwa anaenda kuchukua uhai wa ulimwengu wote, na kuuharibu, na wote walikuwa wenye dhambi, na wamehukumiwa kifo, Kristo alitufia sisi sote. Na Mungu hakuweza kumkiuka Kristo, akiwa Mwana Wake Mwenyewe. Basi Yesu alijitoa Mwenyewe bure, ili Yeye aweze kulipia njia basi kama. . . Musa asingeweza kutenda hivyo. Musa hakuwa na damu ila damu ya binadamu, kama tulivyo. Kwa hivyo, basi, damu yake isingekuwa, isingetosha. Bali Yesu akiwa Damu ya Mungu Mwenyewe, Damu ya uumbaji ya Mungu, Mungu alisamehe tu basi taifa lote la binadamu, dhambi, kwa sababu yote iliwekwa juu Yake. Naye alikwenda Kalvari akafa, nje ya Uwepo wa Mungu, na akateseka. Na akatupwa

kuzimu, kwa sababu kwamba Yeye alikuwa dhambi, alifanywa dhambi zetu. Na hapo pakiwa na m—mchukuzi wa mizigo yetu, alichukua dhambi zetu hadi—hadi Kalvari, na toka Kalvari hadi kuzimu; kisha Mungu akamfufua siku ya tatu, kwa upatanisho wa dhambi zetu.

⁴² Na leo Yeye ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na binadamu, nasi tumeachiliwa bure na kusamehewa. Mungu hata hajui tuliwahi kutenda dhambi. Dhambi zetu ziliwekwa katika Bahari ya Usahaulifu, hazitakumbukwa tena. Hatuwezi kutenda hilo sisi wenyewe; tuna mpaka. Yeye hana mpaka. Na kwa kuwa tuna mpaka sisi, bado tunaweza kukumbuka, kwa sababu sisi si wakubwa vya kutosha. Lakini Yeye ni mkuu mno kwamba Yeye hata husahau tuliwahi kutenda dhambi. Tu wana na binti, Mbele Zake. Na mambo yote ambayo Yeye alikuwa, ndivyo tulivyo. Yeye akawa dhambi yangu, ili kwamba niweze kuwa haki Yake. Akawa dhambi yako, ili kwamba yako. . . Yeye. . . uweze kuwa haki Yake. Kwa hiyo Mungu hawezi kuona dhambi yo yote ndani yako maadamu unamkiri Kristo Yesu.

⁴³ Mtu fulani alisema, wakati fulani uliopita, kasema, “Kama ningeamini kitu kama hicho, jinsi ningefanya ghasia! Ninge vuruga mji kwelikweli. Ningeenda kwenye kila ukumbi wa dansi. Ningelewa, na kila kitu, kwa sababu, . . .”

“Kwa nini?”

“Tayari umemesalimishwa katika Kristo. Inaleta tofauti gani?”

⁴⁴ Nikasema, “Hiyo yaonyesha huna kitu hicho.” Unaona? Kama upendo wa Mungu umegusa moyo wako, katika wema wa Yesu Kristo, ungelimpenda Yeye kiasi kwamba, ulimwengu ungekufa, kama dhambi yako. Hivyo ndivyo unavyojua unaye Roho Mtakatifu. Sio kwa sababu ungeweza kupiga makele, kupaza sauti, kunena, au lugha, au cho chote kile. Bali dhambi inapokufa, nawe u hai katika Yesu Kristo. Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo wa thamani, jinsi ulivyo mtakatifu! Unaona?

⁴⁵ Sasa hapa Louisville, Kentucky, si muda mrefu uliopita, mhudumu alikuwa akizungumza, kwamba kulikuwa na bi—bibi mdogo. Alikuwa amengojea muda mrefu kidogo maishani kuolewa, yapata umri wa miaka ishirini na tano, thelathini. Naye alikuwa msichana mzuri na thabiti wa Kikristo. Na kulikuwa na mtu fulani huko Louisville ambaye hakuwa hivyo, yeye hakuishi maisha mazuri kama hayo. Alikuwa amekimbilia kwenye dansi na majumba ya starehe, na kadhalika, bali siku moja alipata msamaha wa dhambi yake na—naye akawa Mkristo hasa, Mkristo mwaminifu kweli. Yapata mwaka mmoja baadaye, alimpenda bibi mdogo huyu, na bibi mdogo akampenda kupindukia. Basi wakaoana.

⁴⁶ Na baada ya kuishi pamoja kama miaka miwili, wakasema kwamba huyu bibi mdogo alimwambia mumewe siku moja,

akasema, “Mpenzi, nafikiri ni vigumu kwa namna fulani kwako wewe, Mkristo mpya tu,” kasema, “mimi nimekuwa Mkristo tangu ni msichana mdogo.” Lakini kasema, “Kwako wewe, Mkristo mchanga, kumudu hi—hi—hila zote na majaribu yanayoambatana nao baada ya wewe—wewe kufanya dhambi kwa muda mrefu sana.”

Naye akasema, “Vema, inakuwa vita.”

⁴⁷ Akasema, “Nataka ukumbuke jambo moja, kwamba kama adui anakuvuruga mahali fulani, kisha uanguke na kurudi dhambini, usitoroke toka nyumbani. Nataka wewe uje nyumbani.” Kasema, “Nyumbani utamkuta mke yule yule ambaye ulioa.” Akasema, “Nitakusaidia kuomba urudi, na uombe kabisa, upate kumrudia Mungu tena.” Kasema, “Si—si—si—sitaki wewe ukimbie.” Kasema, “Tazama, nilikubali unioe si kwa kutegemea ulivyo wewe, bali nilikubali unioe kwa sababu nilikupenda.” Naye akasema, “Haidhuru unafanya nini, bado ninakupenda. Nilikubali unioe kwa sababu nilikupenda.”

⁴⁸ Na yule mtu siku ile alipoenda kazini, alisikiwa akilirudia jambo hilo katika...mahali ambapo alikuwa akifanya kazi. Akasema, “Basi, mwanamume anaweza kumkosea mtu kama huyo?” Wakati mwanamke, ambaye anampenda sana kiasi kwamba, haidhuru ametenda nini, yuko tayari kurudi amchukue tena, na ajaribu jambo hilo tena. Unaona? Hilo linaonyesha... Sasa, hebu zidisha hilo kwa bilioni na ndipo utapata wazo kuhusu upendo wa Mungu ulivyo. Unaona?

⁴⁹ Kwamba mtu anapompenda Yesu Kristo, vitu vya ulimwengu...Unapofikiria kwa Maandiko kuhusu kile Yeye amekutendea, si kwa mshtuko fulani, lakini kwa nuru ya kweli, jinsi ilivyo, basi kuna kitu fulani kinachotukia ndani yako. Uzao Mpya ujapo, dhambi imekufa kama usiku wa manane. Maadamu Nuru ile iko ndani yako, giza litawakaje? Haliwezi kuwaka. Na hivyo ndivyo ambavyo Mungu alimtendea mtu mmoja ambaye alijitupa kwenye pengo, ambaye aliweza kuchukua ahadi. Naye Musa akiwa m—mfano wa hiki kilicho Asili ya Mfano, hiyo ndiyo sababu Musa alisimama katika pengo kwa ajili ya watu.

⁵⁰ Basi ninashangaa, katika siku hii, ya wakati huu wa Laodikia ulio mpotovu, mzembe na mdhaifu tunamoishi. Sote tunaajua, na tumepitia katika *Nyakati za Kanisa*, kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho, Wakati wa Kanisa wa Laodikia. Na Wakati huu mzembe, mpotovu, usiojali, wenye mizaha, uliojaa dhambi na wa tamaa tunamoishi sasa, ni ajabu kwamba Mungu hasemi tu, “Rudi nyuma, kanisa, nitaliangamiza kundi lote.” Unaona? Wakati wa namna gani tunaishi! Na Yeye atafanya hilo siku moja, pia. Tunajua kwamba inakuja. Hakutakuwa na huruma katika jambo hili, kwa sababu Yeye, tayari, Mtu mmoja alikufa kwa ajili ya wale ambao walitaka kuepuka. Lakini Yeye atachukua wale waliokuwa, au

wamemkubali Kristo na wakawa Wakristo, wataepushwa na ile ghadhabu. Sababu, wakati huo Yeye hakuweza kulitenda; hapakuwa na njia ya kulitenda katika zamani za Musa.

⁵¹ Sasa katika Kitabu cha Ufunuo, tunapofika kwenye wakati wa Kanisa la Laodikia. Katika Ufunuo, sura ya 3, Biblia ilisema kwamba wakati huu, wakati wa Laodikia, ulikuwa “kipofu.” Kasema, “Kwa sababu wewe u ‘tajiri,’ unasema u ‘tajiri,’ na ‘umejitajirisha; makanisa makubwa ya yote, watu waliovalia vizuri zaidi ya wote, makubwa zaidi ya yote yaliyokuwepo katika wakati wo wote.’ Kwa sababu unasema, ‘Sina haja ya kitu.’ Nawe hujui kwamba wewe u maskini, mwenye mashaka, mnyonge, uchi, kipofu, nawe hujui.”

⁵² Sasa kama mtu angekuwa katika hali hii, na ungeweza kumwambia hali yake, angejaribu kujisaidia kama—kama angekuwa na akili timamu. Lakini anapokuwa katika hali ile basi nawe huwezi kumwambia kitu kingine, yeye haamini kabisa kwamba yu uchi, haamini kwamba yuko katika hali hiyo, basi inaonyesha hapa kwamba yeye ni kipofu. Mungu wa ulimwengu huu amepofusha macho ya wale ambao wanakataa kumtumikia Kristo, na wana... ni vipofu sana hawawezi kuona ishara ambayo tunaishi kwake, saa, majira tunamoishi. Basi kumbuka, tayari kuna Mtu anayesimama katika pengo, na hakuna mtu mwingine awezaye kusimama. Au itakubidi kuikubali hiyo dawa, au umekwisha.

⁵³ Sasa, sasa kwetu sisi, kufika karibu sasa na jambo ninalotaka kusema. Tungeweza kuvumilia... Sasa ninajihubiria mwenyewe, katika hili. Tungeweza kuvumilia na kumwona binadamu ambaye ni kipofu, kimwili ni kipofu, naye anajua kwamba anaelekea kwenye genge, je, kama tuna a—akili timamu, kama tulivyvo asubuhi hii, tungeweza kuvumilia kumwona kipofu akielekea kwenye genge, kipofu, na tusijaribu kumuonya? Ingekuwa, hapo, ingekuwa ukatili mno. Tungekuwa wasiojali mno katika moyo wetu. Ungeweza kufikiria, mtu asiyejali sana hata kwamba angeweza karibu acheke, na kumwona kipofu, ambaye hawezi kuona na hawezi kujisaidia mwenyewe, kwa makusudi aende akielekea kwenye genge? Hicho kingekuwa ki—kitu kibaya; na asitende neno.

⁵⁴ Vema, kwa ndugu zangu, ulimwenguni pote, nataka kuungama jambo hili. Kwa—kwa unyenyekevu nitasema hivi, kwamba hilo ndilo nililokuwa karibu kulitenda, au nililokuwa nikitaka kufanya. Nimekuwa nikihubiri kwa miaka kadha, na ni—nimekuwa mzee na mhubiri mzoefu wa zamani, na nimekuwa na vita vingi vigumu, na labda nimetiwa kovu, nimekatwakatwa kila mahali mle ndani, kutokana na vita. Kwa sababu, fungu langu, ambalo Bwana alinipa, si kule nyuma kuwabusu watoto wachanga, na—na kuoza vijana, na kuzika wazee. Bali ilikuwa kushika Upanga wenye makali kuwili katika mstari wa mbele vitani, dhidi ya hila za—za upagani na elimu

ya pepo, na—na nguvu za giza, na kupigana kwa Neno la Mungu mpaka nimeona adui ameshindwa. Nimepata majeraha mabaya, mara nyingi.

⁵⁵ Halafu nilipokuja na Ujumbe katika siku hii, na kuliambia kanisa mambo ambayo ninataka kuyasema. Nami nilibashiri miaka mingi iliyopita, Roho Mtakatifu aliponiita kwenye kazi hii. Na hakuna mtu anayeishi duniani leo, ambaye angewahi kusema kwamba Bwana aliwahi kuniruhusu niwaambie cho chote katika Jina Lake, ila ambalo lilitimia sawasawa namna lilipaswa litendeke.

⁵⁶ Jinsi Yeye alivyonituma mimi kwanza, na kipawa cha kwanza, na kipawa cha pili, na mambo ambayo yamenenwa au kutendeka, duniani kote, na kwa dhahiri mamilioni wamemjia Kristo. Na makumi elfu ya wahubiri wametiwa moyo, jambo ambalo limeanzisha ufufuo ambao umefagia uso wote wa dunia leo. Na kwa kuwa Wapentekoste ndio walioupokea Ujumbe wangu, ndio ambao wamesonga mbele. Kanisa la Kipentekoste linaonyesha waongofu wengi zaidi katika kundi dogo la Wapentekoste kuliko makanisa yale mengine yote yakiwekwa pamoja. Hizo ni takwimu. Kwa nini? Kwa sababu ya wao kupokea Ukweli na kupokea uamsho.

⁵⁷ Na sasa, baada ya wakati mkuu kuja wa kuponywa wagonjwa, kutoa pepo, na kufufua wafu; jambo ambalo sote tu mashahidi, na hivyo pia madaktari wengi na watu maarufu wa dunia. Na kutokea kwa Bwana Yesu miongoni mwetu, kama mnavyoiona hiyo ishara pale, nadhani ukutani, po pote ilipo, ya Malaika wa Bwana. Na jinsi wanasayansi wameichukua nakala yake wakihalalisha, na ni—ni ukweli unaojulikana, ulimwengu mzima. Na kuona mambo yale hasa ambayo Yeye ameyatenda, yakitokea, kila wakati. Basi, ikiwa Nguzo ya Moto ambayo ilikwenda pamoja na Israeli kuvuka jangwa, katika siku za Musa, ambalo sisi . . . au sasa kwamba Musa aliitwa, “Mtumishi wa Bwana,” na yeye alifuata Nguzo ya Moto usiku, na Wingu mchana.

⁵⁸ Na wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alisema Yeye ndiye aliyekuwa Mungu yule. Alisema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Na “MIMI NIKO” ndiyo ile Nguzo ya Moto iliyokuwa katika kijiti kilichowaka moto, iliyonena na Musa katika si—siku zilizopita. Nafikiri hilo ni sahihi, ndugu Vayle. Halafu Yeye alisema, “Ninatoka kwa Mungu Nami narudi kwa Mungu.” Ndipo aliposulubishwa, akafa, na akafufuka, na akapaa huko Juu, na akalaza mwili Wake juu ya madhabahu kuu ya Mungu wa Milele, apate kuwepo pale sikuzote kutenda badala yetu, kujua kwamba Yeye amelipa deni yetu ya dhambi. Na hapo akarudi duniani tena katika umbo kuu la Nguzo ya Moto.

⁵⁹ Mtakatifu Paulo, akienda zake, kabla ya yeye kuitwa Mtakatifu Paulo, aliitwa Sauli wa Tarso. Basi alipokuwa akienda

zake Dameski, kuwakamata watu fulani ambao walikuwa wanafanya makelele mengi sana, na kupaza sauti; na kuhubiri Injili ambayo ilikuwa kinyume cha desturi za makanisa yao. Alipokuwa anashuka kwenda zake, siku moja, wakati kama huu mchana, alipigwa na Nuru kuu akaanguka chini. Na Nuru hii kuu, yeye akiwa Myahudi na anajua kwamba ile Nguzo ya Moto iliwaongoza wana wa Israeli, na Hii hapa mbele yake tena, alipaza sauti, “Bwana!”

⁶⁰ Sasa kama mkichunguza katika tafsiri zenu katika King James na Standard zenu pia, na kadhalika, ni herufi kubwa B-w-a-n-a. Na mtu ye yote ambaye anajua Biblia yake, anajua kwamba wakati hilo B-w-a-n-a likiwa katika herufi kubwa, ni Elohim, Mtu ajitoshelezaye kwa yote ambaye aliumba mbingu na nchi, katika Mwanzo 1:1. Unaona, ni herufi kubwa, “Bwana!” Sasa Paulo asingaliita madanganyo fulani ya macho, asingeita kitu fulani asichojuwa habari zake, kwa sababu alikuwa mtu aliyefundishwa katika Maandiko. Alifunzwa na Gamalieli, mwalimu maarufu wa zamani zile, na asingeita hiyo, “Bwana,” kama hakuridhishwa kwamba huyo alikuwa Yehova. Alisema, “Bwana, U nani Wewe?”

⁶¹ Sikilizeni Sauti ile ikimjibu, “Mimi ni Yesu,” yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁶² Kwa hiyo nafikiri, katikati ya yote hayo, kabla ya kwenda mbele zaidi, sehemu zote mbili hapa na ulimwenguni pote, watu watakasikiliza, na wanasikiliza sasa, watajua kwamba imethibitishwa kwa kila kitendo kuwa ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Katenda mambo yale yale ambayo Yeye alitenda, akawaponya wagonjwa, alijua mawazo ya akilini, kwani hilo lilionyesha mambo ambayo yangetokea, na kila wakati kikamilifu katika miaka hii. Nina umri wa miaka hamsini na minne, na nimeona maono tangu nilipokuwa na umri wa miezi kumi na minane, na, hapana hata wakati mmoja, bali kila wakati imekuwa kweli. Unaona? Sasa, hiyo lazima iwe ni Mungu. Na halafu mimi nikifikiria jambo hilo, “Kwa nini watu ni vipofu sana kwamba hawawezi kuona jambo hilo?”

⁶³ Na wakati wote ninapozungumza na na—na wanawake wetu kuhusu kukata nywele zao, na wahudumu wakinipigia makelele kuhusu jambo hilo; na kuhusu wao kuvaa nguo chafu, za hizi kaptura, na—na kuishi hivyo, na—na kuendelea katika njia hiyo mbaya; na kuhusu wanaume wetu namna walivyokuwa wakifanya, wakivuta sigara, na kunywa pombe, na—na kila kitu; nao bado wanajiita wenyewe Wakristo, na kushiriki Meza ya Bwana mezani kwa sababu eti wao ni washiriki wa madhehebu. Loo, kwa kweli, walifikiri nimemkufuru Mungu. Na hivi wanawake wamekuwa bora zaidi? Walizidi kuharibika, kote tifani.

⁶⁴ Halafu mimi, nikiwa na wasiwasi, (na nena hili kwa namna fulani kimya kimya), hivi pengine ni mtu aliye na wasiwasi wa akili, na nikijua kwamba nilikuwa sijitoshelezi, hapo mwanzoni, kwa kazi hii; kwa vile wengi wamelalamika, kwa kufanya hivyo. Ilikuwa ni vigumu. Lakini ni—nilifikiri, “Mungu, kwa nini Wewe hukumwita mtu fulani ambaye angeweza kulitenda. Nami ni—ninasikitika, lakini ni—nimeshindwa. Watu hata hawatanisikiliza. Nami nimeshindwa kufanya jambo ambalo ingelinipasa kufanya, mahali fulani, kwa sababu hawatasikiliza.”

⁶⁵ Mama yangu, ambaye hivi karibuni amekwenda Utukufuni, yapata—yapata zaidi ya mwaka mmoja uliopita. Mama yangu, baba yake alikuwa mwi—mwindaji. Nami nafikiri nilipata yote hayo toka kwake, katika msimamo huo, sababu na—na—napenda misitu. Nami nikafikiri, “Kama watu hawa ambao wanajiita wenyewe Wakristo, kama hawataki kusikiliza Ujumbe ambao ninauhumbiri, basi na wakae. Nitauacha tu, kabisa, kisha nitaenda mlimani. Na najua rafiki ambako. . .” Wengi wenu, hapa, mnakumbuka mimi nikibashiri wakati, yapata miezi sita kabla haijatokea, jinsi ambavyo ningeenda mahali fulani, moja kwa moja toka kwenye jukwaa hili hapa, na kungekuwa na m—mnyama anayefanana na kulungu mwenye pembe zenye ncha kali, na jinsi ambavyo zingekuwa inchi arobaini na mbili, na jinsi kungekuwa na dubu wa rangi ya fedha mwenye urefu wa futi saba. Mnalo kwenye kanda na kila kitu. Nadhani kwamba mnakumbuka wakati huo, ninyi nyote. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, liko kwenye chumba changu juu kule sasa, ku—kuonyesha kwamba ni kweli.

⁶⁶ Sasa katika mambo kama hayo, kwa sababu ni kabla tu ya kufariki kwa mama yangu, na Yeye alikuwa akitaka kunituliza kwa ajili ya huo msiba mkubwa, kwa kuwa Yeye alijua kwamba angemchukua.

⁶⁷ Sasa, nilikutana na mtu aliyekuwa Mkristo, naye anayo ardhi pana kule chini karibu sana na Alaska. Nami nilikuwa nimeamua, kwamba kwa vile nimeondoka hapa na kwenda Magharibi, kwamba ningemchukua mke wangu na kwa namna fulani nimnase kwenye jambo fulani; ningemchukua juu kule, nami ningekuwa kiongozi. Na halafu kama Bwana alinitaka nifanye jambo fulani, ningeachilia nywele zangu zikue na—na ni—ninge. . . masharubu yangu. Na—na ni—ningerudi hapo na kuwa kiongozi. Kuna Wahindi kama wawili watatu wanaoishi nyuma huko mbugani. Mimi—mimi ningekuwa tu kiongozi na kumsaidia Bud. Na kama Bwana alinitaka mimi nifanye cho chote, basi ninge—ningesema, “Sawa, Bwana.” Yeye angenipa ono. Ningeondoka niende kisiri.

⁶⁸ Ninasema watu. . . Sijawahi kamwe kujihesabu mwenyewe, mtu ye yote akijua jambo hili, bali watu wamesema, “Ndugu Branham, Bwana amekuita kuwa nabii Wake.” Vema, mimi—

kamwe sijajidhania kuwa hivyo, bali nilianza kufikia wakati ambapo nilikuwa tayari karibu kulitenda, kufikiri, “Vema, pengine ndivyo nilivyo. Kama mimi ndivyo nilivyo, nitaishi kule nyuma nyikani. Na iwapo nitaishi kule nyikani, basi nita—nita—nitakuwa nabii Wake, unaona, na basi kama Yeye anataka kunipeleka mahali fulani. Na wakati Yeye hanitumii, basi hakika nitavua samaki wazuri na—na kufanya mambo fulani.” Bila shaka, hiyo ilikuwa nia ya kujipenda, unaona, kwa sababu nilipenda kutenda jambo hilo. Naam, hilo hasa silo jambo lipaswalo kutendwa. Na sasa nilikuwa nimeamua akilini mwangu kulitenda hilo.

⁶⁹ Na sasa, kabla tu zile *Nyakati Saba za Kanisa* kuhubiriwa, kama zilivyochorwa pale... Wapo wengi, leo, ambao walikuwepo hapa wakati ule, na wanajua jinsi Bwana alivyolibariki jambo hilo, kwenye ukuta nyuma huko, Huo uliorudisha nuru yake. Ili tu... Wangapi wapo hapa sasa, ambao walikuwa hapo wakati ule Yeye—Yeye alipokuja? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hilo lilitendeka.

⁷⁰ Basi ninakumbuka wakati huo kuhusu Ndugu Jackson. Yeye kwa kawaida yu pamoja nasi. Ndugu Junior Jackson, yule Mmethodisti alikuwa mhudumu wa Kimethodisti. Ndiyo, yupo hapa ameketi hapa sasa. Sasa, kwamba alinjia na ndoto, na halafu baadhi ya ndugu wengine walikuja na ndoto kama zile. Sasa, Bwana amekuwa mwema sana kwangu, na sijawahi, nawatakeni mshuhudie asubuhi hii, je, nimewahi kuwaambia tafsiri baya ya ndoto. La, bwana. Kwa sababu, kwamba Bwana... Sitasema habari zake mpaka niione tena na kujua Yeye anasema nini kuhusu jambo hilo, ndipo nitakuambia. Basi akasema ni—nilikuwa ninaendesha ibada kule chini kwenye kanisa lake, naye, kwa namna fulani au nyingine, alikuwa na wasiwasi mno usiku ule, naye akatoka kanisani akakimbia akaja upande ule mwingine akanikuta kwenye gari, huku watu wanapita karibu nami. Kasema, “Nataka kukuambia jambo fulani.”

⁷¹ Basi akaniambia kwamba aliota ndoto, kwamba juu hapa mahali fulani, kama Indiana, kwamba kulikuwa na kilima kikubwa kirefu, chenye manyasi, na maji yameuzoa udongo wote ulio juu, na kikawa mwamba ka—kama kilele kitupu juu ya—juu ya mlima. Basi katika mwamba huu kulikuwa na Maandishi ya ajabu. Ndipo akasema nilikuwa nimesimama pale na ndugu wote wa kanisani hapa, nikitafsiri Maandishi haya. Na kisha ilipofikia wakati ambao nimemaliza kuyatafsiri yote, ndipo ile... kwa namna fulani au nyingine, iwapo ninaifahamu ile ndoto vyema, nilishika kitu kama mtaimbo, au—au aina fulani ya mtaimbo wenye pembe au kitu fulani, au mtaimbo wenye pembe, nilimaanisha m—mtaimbo wa kuvunjilia au kitu fulani, basi nikakata kilele cha mlima ule na kukiinua juu. Basi ndani yake kulikuwa na mwamba mweupe, kitu kama namna ya jiwe

gumu sana au—au kitu kama hicho, mwamba mweupe ambao haukuandikwa. Nami niliwaambia wale ndugu, “Kaeni hapa mkiangalia ndani ya Hili.” Basi mimi, wakati wote walipokuwa wanaangalia, nikaondoka kisirisiri miongoni mwao nikaanza kwenda Magharibi. Naye Ndugu Jackson alisema kwamba aliniona nikivuka kilima kimoja, na halafu kilima kingine, nikizidi kuwa mdogo zaidi na zaidi, nikielekea Magharibi. Mnakumbuka jambo hilo.

⁷² Vema, tafsiri yake, bila shaka, ilitolewa hapa kanisani kabla ya kutokea, kwamba ule—ule wakati ndio huu sasa, ambao ninaamini, kwamba ufunuo wote kupitia wakati wa Luther, Wesley, na John Smith, Alexander Campbell, na wengine mbalimbali ambao wamehubiri juu ya Biblia, na halafu tulifika kwenye Biblia na kuonyesha kwamba kungekuwa na U—Ujumbe wa malaika wa saba. Na katika kupigwa kwa baragumu ya Ujumbe wa malaika wa saba, siri zote za Mungu zingejulikana. Ndipo zitakuja zile ngurumo saba za siri.

⁷³ Na sasa kama ni wakati ule wa mwisho ambao tunaishi, ambapo tumepanda toka kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; na tumekuwa na ishara, maajabu, na mambo yote mbalimbali. Na zile karama zimerudi kanisani, kama vile, uponyo wa Kiungu, na unabii, na—na kunena kwa lugha, na tafsiri. Na ingawa zimeelezwa vibaya, vya kutisha, bali hata hivyo, hilo haliondoshi, kuna zilizo nzuri. Kuna iliyo kweli, iliyo halisi, kipawa cha kunena kwa lugha, ambacho kinapaswa sikuzote kuwepo Kanisani.

⁷⁴ Tunao waigizaji wengi. Tunao watu ambao wanainuka na kujaribu kutenda kama Wakristo, nayo maisha yao hayalingani, kwa hiyo kuna kosa fulani. Yesu alisema, “Kwa matunda yao mtawatambua.” Unaona? Hivyo ndivyo unavyomjua Mkristo, jinsi anavyoishi. Usiruke kamwe juu zaidi ya unavyoishi. Kwa hiyo basi hebu... Bali katika hilo, lakini ni she—ibilisi akitengeneza kitisho, kuzuia waamini halisi na wa kweli kukaribia jambo la kweli la Hilo. Lakini Mungu na atusaidie kujitenga na kuweza kupambanua kati ya kweli na uongo. Na—na Neno sikuzote litanyosha hilo.

⁷⁵ Sasa tunaona kwamba, katika jambo hili, niliwaambia ninyi jambo hilo, tafsiri ile juu ya Mwamba ule. Na Mwamba ule ni Kristo, ambao ulikuwa katika ndoto ya yule ndugu, na hilo ni Biblia. Na kwa miaka yote hii, Biblia imefasiriwa, mpaka tumeipa Hiyo tafsiri ya kidini kabisa. Na kipawa cha mwisho kikiongezwa katika wakati wa Laodikia, ambacho ni wakati wa malaika wa saba kuhubiri, katika wakati wa Laodikia, wakati ule ambapo kungekuwepo na mambo mengi ambayo yemefahamika vibaya nyakati zilizopita.

⁷⁶ Kama Luther alivyohubiri kuhesabiwa haki, bali akakuachia kukapotoshwa kwa sababu hakuishi muda

mrefu vya kutosha. Na halafu...Halafu wakalifanya kanisa madhehebu. Luther hata kamwe hakulifanya madhehebu; baada ya Luther. Na halafu Wesley akatokea. Na baada ya Wesley, wakapata kanisa la Wesley. Na halafu baada ya hilo kukaja John Smith, Mbaptisti; halafu Alexander Campbell, na kadhalika. Lakini hao watu, hao watengenezaji, hawakuishi kirefu vya kutosha kuyakusanya yote pamoja. Na kwa hiyo tuna sehemu nyingi zinazolegalega, yaonekana. Na halafu wakati walipofanya hayo, kwa mfano, kama ubatizo wa maji ambao John Smith alirejesha, ubatizo wa maji katika—katika kuzamisha; lakini akitumia cheo. Na mengi ya mambo hayo ambayo yaliachwa yamelegalega. Na basi tunapofikia mwisho, Ujumbe wa mwisho unapaswa kunyosha hayo yote, kuleta mambo haya kwenye “imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja.” Unaona?

⁷⁷ Na sasa baada ya Biblia kwisha kufasiriwa, kabisa, ndipo unaona kilifunguliwa kilele cha Mwamba ulio kama piramidi. Si fundisho la piramidi sasa, sio hilo, kwa sababu mimi... Mtu anayefundisha fundisho hilo la piramidi, nadhani wanajua ambalo wanazungumzia. Mimi sijui neno kuhusu hilo. Bali, hata hivyo, ulikuwa katika umbo la piramidi, lakini kile kifuniko juu ya hiyo piramidi kamwe hakikuwekwa. Nimekuwepo Cairo na—na Misri, na—na kile kifuniko kamwe hakikuja, kwa sababu kilikuwa jiwe la pembeni, lilikuwa jiwe la kichwani. Katika kanisa lilikuwa jiwe la pembeni. Katika Kanisa lote kamili, Hilo lilikuwa jiwe la kichwani. Kwa hiyo Hilo halikuja kamwe. Hilo lilikataliwa, Kristo. Nalo litakuja. Nami naamini kwamba wakati Hilo linakuja, kwamba kanisa litaumbika hadi mahali fulani, toka kuhesabiwa haki chini ya Luther, kutakaswa chini ya Wesley, na ujumbe wa Kipentekoste utalifikisha kanisa kwenye uchache sana, na huduma itakuwa miongoni mwa watu hao mpaka itakuwa huduma ile ile aliyokuwa nayo Yesu Kristo. Hilo litamleta Yesu na kuwanyakua wote.

⁷⁸ Wote hao Waluteri, Wapresbiteria, Wabatisti, Wamethodisti mwaminifu na wa kweli, na ye yote yule aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, watanyakuliwa pamoja na Yesu Kristo hapo atakapokuja. Ninaamini hilo. Ninahitilafiana na baadhi ya ndugu zetu wa Kipentekoste wanaoamini kwamba masalio ya kanisa ndio watakaonyakuliwa katika wakati huu wa mwisho. Ninatofautiana nao hapo, kwa sababu Mungu... Mtu angeweza, na Mungu angeweza... Kama tungesema, “Yeye angeweza?” Yeye anaweza kufanya lo lote analotaka. Lakini Mungu, aliyemwahidi Luther, na chini ya kuhesabiwa haki, hilo ndilo tu walilojua. Unaona? Yeye aliahidi kulichukua Kanisa. Na Yeye... Ninaweza kuamini kwa neema ya Mungu na kwa kuungwa mkono na Maandiko. Kwa sababu, Yeye hakuja katika zamu ya kwanza, nao wakalala; na zamu ya pili; na kuendelea. Katika zamu ya saba, Yeye akaja. Na huo ni Wakati wa Saba wa

Kanisa, kwenye Ujumbe wa malaika wa saba. Unaona? Na hapo alipokuja, wanawali hao wote waliamka wakazitengeneza taa zao. Mpresbiteria, Mluteri, Mbatisti, ye yote ambaye amezaliwa kwa Roho wa Mungu, atanyakuliwa. Ninaamini kwamba Bibi-arusi ataitwa wakati ule. Ninaamini kuna wengine katika siku za mwisho haitawalazimu kuonja kifo, bali watabadilishwa mara moja, kufumba na kufumbua.

⁷⁹ Sasa, kama mlivyoona, katika ndoto ya Ndugu Jackson, kwamba hakukuwa na maandishi juu ya Mwamba huu kwa ndani, hilo ndilo nililoenda Magharibi. Sasa, kama ilivyotukia, kisha nikawaambia, siku moja ningewaambia ilichomaanisha. Nimekwenda Magharibi kwa ajili ya jambo hilo. Nami nikawaambia ninyi ono lile ambapo watu, kwenye kanda na pia waliopo asubuhi hii, watajua wakichukua *Je, Mabwana, Ni Wakati Gani?* Na ye yote wenu ninyi ndugu wa kanda ambaye hana Ujumbe huo, naye anataka kufuata Hili, chukua: *Je, Mabwana, Ni Wakati Gani?* Hapo kabla, majuma na miezi kadhaa kabla haijatendeka, hapa niliona ono la kuweko Tucson, kaskazini mwa Tucson; hiyo ingekuwa mashariki mwa Flagstaff, kaskazini mwa Tucson; na ningekuwa ninaoondoa vichomanguo kwenye miguu ya suruali yangu na m—mlipuko ungelipuka ambao kwa kweli ungeonekana kama ulitikisha nchi. Ni wangapi wenu wanakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema “Amina.”—Mh.] Hilo ni kweli. Ambao ungetikisa nchi.

⁸⁰ Vema, inatukia kuwa basi mtu mmoja yupo asubuhi hii ambaye alikuwa anasimama pale lilipotukia. Huo kwa kweli ulitikisa miamba ikaporomoka kwenye mlima. Na sasa wao... Tunaona kwamba, kwenye wakati huo, niliona Malaika saba katika—katika umbo la piramidi, ambao walishuka kwa kasi na kunichukua juu. Nami nililetwa Mashariki, kufungua zile Muhuri Saba za Mungu. Kama hauna hizo... Kama Yesu akikawia, nami... vitukuu vyangu, watoto wa mtoto mchanga Paul, hilo bado litakuwa Kweli ya Milele ya Mungu aliye hai. Sasa, hiyo ilikuwa ni kutafuta, kile kilichotiwa muhuri ndani ya mlima huu, ambacho hakikuandikwa. Ilipaswa kitafsiriwe. Na niliporudi, Malaika wa kwanza, usiku wa kwanza, alifungua Muhuri kinyume cha kitu cho chote tulichowahi kusikia katika maisha yako. Na zote saba zilitokea namna ile ile. Mnajua hivyo. Mlikuwego hapa wakati lilipotukia, wengi wenu.

Na, sasa, sikulijua wakati ule, bali . . .

⁸¹ Ndugu Fred Sothmann, najua yupo hapa. Na nina hakika kabisa Ndugu Norman yupo hapa. Tulikuwa kule juu... Ilinipasa kwenda Houston kuhusu kumwokoia yule kijana na kunyongwa kwa kiti cha umeme. Na halafu nilirudi nikaenda kuwinda juu kule pamoja na wale ndugu. Na asubuhi ile, nilikuwa nimesimama pale nikiondoa vichomanguo, au—au wanavyoita *vichwa vya mbuzi* kule, vichomanguo kwenye mguu

wa suruali yangu. Na mlipuko ule ulifanya vile vile tu jinsi Huyo alivyosema. Hilo ni kweli, Ndugu Fred? Nami—nami—nami lazima niliruka juu sana toka ardhini. Na juu yangu kidogo tu walikuwepo Malaika wa Bwana ambao waliouleta ule Ujumbe, kwamba nije humu nikazivunje Muhuri hizi. Kwa nini hapa, kwa nini kwenye Maskani? Kwa nini sikulitenda hilo kule? Kwa sababu nilifanya ahadi kwa kanisa langu na kwa Mungu, kwamba Ujumbe wo wote mpya ungetokea kwenye Maskani hii, ungerokidwa toka hapa. Na Yeye alikuwa akinisaidia kudumisha neno langu, kukaa nyuma hapa kulitenda. Na halafu mara moja nikarudi tena.

⁸² Na, sasa, sikujua wakati ule, kwamba walikuwa wanapiga picha zake, wanasayansi walikuwa wanazipiga, Malaika wale walipojishusha toka Mbinguni, kuleta Ujumbe. Na mnakumbuka, nilisema yule Mmoja upande wa kuume wa kundi lile alikuwa, kwa namna fulani, amerudisha kifua Chake nyuma, na mbawa Zake. Mnakumbuka mimi nikisema hivyo, ninyi nyote? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Na jinsi ambavyo nilimwangalia Yeye? Yeye alikuwa anaonekana dhahiri sana kuliko hao wengine. Nami sikujua walikuwa wanachukua picha Yake, sababu mara niliharakisha nikaenda Mashariki. Lakini nikirudi nyumbani Tucson, Hilo hapo lote katika magazeti ambalo limekwisha onekana karibu nchini kote, au hadi Mexico, na Mikoa yote ya Magharibi, na nafikiri Courier hapa. Lilikuwa kwenye Associated Press. Wangapi waliona, “Wingu la ajabu angani?” Mnaona mikono hiyo. Na sasa gazeti la *Life* liliichapisha. Na nina na—nakala hapa asubuhi hii, katika gazeti la *Life*, la kuonyesha. Hili hapa sasa, wakati ule ule nilipokuwepo kule. Unaona piramidi ya hilo Wingu? Nilikuwa nimesimama chini kidogo tu ya hili. Na hapo, unamuona yule Malaika anayeonekana dhahiri upande wa kuume? Unaona ubawa Wake uliochongoka? Sawa kabisa na ambalo lilisemwa. Na hapa lipo linaonekana Mexico na sehemu mbalimbali toka ambapo walipiga picha ile. Sasa, huyu mwanasayansi hapa anajaribu ku—kupata maelezo yote kuhusu picha hii, awezayo kupata, kuhusu watu walio na picha hii. Anaichunguza.

⁸³ Sasa, anasema hapa kwamba isingewezekana kwa hilo kuwa wingu, kwa sababu unyevu hauendi juu yapata, ningesema, kama maili sita au nane kwenda juu, kitu kama hicho. Tunapoenda ng’ambo kwa kawaida tunaruka futi kumi na tisa elfu, na tuko juu ya tufani wakati huo. Bali wingu hili, kulingana na makala haya hapa ya huyu mwanasayansi liko maili ishirini na sita kwenda juu. Hilo lingekuwa maili na maili mbali na unyevu. Basi yeye alisema, akichunguza ile sehemu, na sasa, mnajua mimi. . . Wangapi wanakumbuka kwamba niliwaambia, “Ilisikika kama sauti ya kishindo kikuu cha ndege”? Mnakumbuka? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Lakini hakukuwepo na ndege wilayani. Kitabu kinasema

hivyo hapa. Wamelichunguza jambo hilo. Hapakuwepo na ye yote, hakuna ndege kule juu. Na, isitoshe, isingewezekana. . . Ule ukungu nyuma ya ndege si cho chote ila unyevu wa hewa iliyovunjika-vunjika, unyevu, sababu hunyonywa kupitia kwenye mtambo huu, kama jeti. Wakati inapojivuta yenyewe, huvunja-vunja unyevu hewani. Haiwezi kuuondoa, maadamu kuna jeti, kwa sababu yabidi ku. . . Huo ndio unaoisukuma mbele, na ni unyevu unaotoka mbio kwake.

⁸⁴ Bali hili hapa, maili nyingi juu ya sehemu inayoweza kupata unyevu, na hakuna ndege wilayani. Basi Huo usingeweza kuwa unyevu kule juu, na uning'inie kule siku ile. Upana wake ni maili thelathini, maili ishirini na sita kwenda juu. Unaona? Vile vile tu kama ilivyokuwa picha ile *pale*, wakati nilipowaambia, “Malaika wa Bwana alionekana kama Nguzo ya Moto,” miaka mingi iliyopita, kabla haijapigwa picha. Mungu huifanya sayansi itambue kwamba Hilo ni Kweli. Na hapa, kuhusu ule utabiri uliotolewa, Mungu anaifanya sayansi ishuhudie kwamba Hilo ni Kweli. Sasa unatumama wapi? Nataka kuliweka hili, kwani na—naweza nizungumze na rafiki yangu, ambaye yupo asubuhi hii, ku—kuandika zile *Muhuri Saba*. Pengine angependa kutumia hili kwa ajili ya hilo. Na kwa hiyo unayo nakala yake, mbona, kama ukipata moja, iweke upate kuiangalia. Unaona?

⁸⁵ Sasa anataka kujua, lakini ya nini kwenda kumwambia jambo hilo? Angelilicheka. Unaona, angecheka tu. Kwa hiyo hatutupi lulu zetu namna hiyo. Bali tunajua, kanisa linajua, na Mungu anajua kwamba ni Kweli.

⁸⁶ Na basi nilipokuwa ninaomba juu ya jambo hili, la kushangaa nini kingetukia kwangu, nanyi mnaajua nilikuwa wapi? Kasakazini mwa Tucson, mashariki ya Flagstaff; sawasawa kabisa, mahali panapofaa, ambapo niliwaambia, iwezi kadha kabla hayo hayajatukia, ningekuwa nikisimama. Na sawa kabisa kulingana na gazeti hili hapa, na kuhusu magazeti ya kila siku na gazeti hili, na ushuhuda wetu, mahali pale pale lilipotukia. Mungu ni mkamilifu na hawezi kudanganya, na itatimia.

⁸⁷ Mnakumbuka katika kanda: *Je, Mabwana, Ni Wakati Gani?* Nitalikariri tena, “Kumbukeni, kitu fulani kiko karibu kutokea, kitu muhimu sana.” Na sasa Hilo limelifanya taifa nzima kushuhudia jambo Hilo. Kila gazeti katika Associated Press, na moja ya magazeti yetu yanayoongoza, na mengine yote, yanashuhudia habari Zake, na halijasambaa kila mahali, bado. Bali sisi ni watu waliotunukiwa baraka jinsi gani, wa—watu waliojaliwa ambao ni Wakristo, kujua kwamba katika saa hii yenye giza, wakati hakuna matumaini kulingana na sayansi, kombora la atomiki linatungojea. Na hakuna matumaini katika madhehebu yetu, ya daima yanaungana, wanajiimarisha kwa alama ya mnyama. Na wakati matumaini yetu yote kwa upande huo yamekwisha, katika uchumi wetu, juu ya ushirika wetu wa

Kikristo katika madhehebu. Inaelekea kwenye Ukatoliki, ambao utakuwa alama ya mnyama katika ule muungano wa makanisa.

⁸⁸ Lakini, na wale wanaompenda Mungu na wanatazamia ukweli, Mungu yule yule aliyefanya ahadi katika Biblia, amelienza mbele ya uso wetu; na kulifanya kanisa, na watu, na sayansi, na magazeti, na kila kitu, kutambua kwamba Yeye bado ni Mungu naye anaweza kutimiza ahadi. Wakati wa jinsi gani!

⁸⁹ Ndipo nikiwa mle Sabino Canyon asubuhi ile, nikiomba na kushangaa nini kingetukia, nikimwinulia Mungu mikono yangu, kule juu kwenye kilele cha mlima ule, Upanga ule uliangukia mkononi mwangu; wenye mpini wa lulu, na kifuniko chake, na bapa lake lenye urefu wa kama futi tatu, na unametameta kama bati la sufuria au kama chuma inayong'aa sana, mkali kama wembe. Nami sikujua ilikuwa ni nini. Ndipo nikasema, “Ninaogopa vitu hivi.”

⁹⁰ Na mara hiyo Sauti ikanena, ambayo ilitikisa lile genge. Kasema, “Huu ni ule Upanga wa Bwana.” Na Upanga wa Bwana ni Neno la Bwana, kwani Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili.

⁹¹ Halafu nikirudi nyuma kwenye jambo hilo, basi, wakati huo, ndugu mdogo shujaa hapa kanisani . . . Basi yeye alikuwa askari naye karibu alifumuliwa vipande-vipande jeshini, na akaachwa hapo afe, ndipo kasema ange . . . Hawakudhani, madaktari hawakudhania angeishi, na hata hakuwa mtu anayefaa kushughulikiwa, alikuwa mahututi sana. Mishipa mikuu katika mguu wake ilipasuka; mkono wake mdogo karibuni ulifumuliwa kabisa; mguu wake, mguu mmoja karibu umekatika. Bali Mungu aliona neema, akamwokoia na akamponya siku moja.

⁹² Yeye, ndugu Roy Roberson, alikuwepo wakati picha ile ilipopigwa kule Houston. Jinsi mkewe alivyoambiwa kwa ono, alichokuwa akitenda mchana, na jinsi alivyokuwa na shida na ingeponywa. Na hilo lilimfanya mwamini. Bali yeye, akiwa mwanajeshi alikuwa kwa namna fulani, (natumaini atanisamehe kwa kusema jambo hili) kutoka ambapo yote yale—upande wa ukali, utaratibu, akitoa amri jeshini. Kama mwenye amri kwa wanadamu, ilimbidi kuamrisha kwa ukali, na, “Fanya hilo!” Unaona? Na yeye—yeye aliamini, hata hivyo. Bali kidogo kidogo, huku akihudhuria kanisa na kuona ya kimbinguni, alisema, “Ninaamini hilo, lakini hilo ni kwa ajili ya mtu mwingine.”

⁹³ Bali usiku mmoja Bwana alimwamsha, asubuhi moja. Tulikuwa tumeketi, mimi na yeye, ilionekana kama huko Yerusalemu katika Meza ya Bwana, nami nilikuwa ninazungumza. Hakuweza kuelewa. Na Ndugu Roy, anayeketi humu sasa, akiniangalia moja kwa moja sasa hivi, yeye aliliona. Ndipo akanipigia simu, huko Houston . . . au nje huko Arizona, au alinipelekea barua nami nikampigia simu. Akasema, “Ulikuwa umeketi pale, Ndugu Branham, nami nikaona ile

Nguzo kubwa ya Nuru ikiingia na kukuchukua, na ikakuchukua ikakuondoa kwenye meza ya Bwana, nawe ukaenda zako upande wa magharibi,” Bila shaka alikuwa ameketi upande wa mashariki akiniangalia mimi nikienda magharibi, na Nuru hii iliingia na kunitoa nje.

⁹⁴ Kasema ilikuwa usiku mmoja, ilikuwa katika ono. Katoka kitandani, kama saa tisa au kumi usiku, kitu kama hicho, na akaona jambo hili likitukia. Basi kasema alipiga mayowe, ilionekana, kwa siku nyingi, “Ndugu Bill, rudi!” Basi mimi na Roy tumekuwa ndugu kwelikweli. Tunaishi pamoja, na kuwinda pamoja, nasi ni ndugu tu. Ndipo aka—akapiga mayowe kwa ajili yangu, mpaka akaishiwa na sauti kooni mwake, “Rudi! Mrudishe! Mrudishe,” akilia. Akasema ni... Hapa ikaja ile Nguzo ya Moto ikirudi, au Wingu lilirudi, na Yeye akaniweka mbele ya meza, nami nilikuwa nimekwisha badilishwa. Ilikuwa ni jambo lisilofahamika kwa Ndugu Roy, mimi kubadilishwa, kuonekana tofauti. Naweka hiki juu hapa kwa ajili ya kitu ninachotaka kukumbuka, “kuwa nimebadilishwa,” nilipompa yeye tafsiri yake.

⁹⁵ Hiyo ilikuwa kabla tu sjarudi kwa ajili ya zile Muhuri Saba. Niliporudi kwa ajili ya zile Muhuri Saba, basi mimi. . . Asubuhi moja alimshika Billy, naye alitaka kuongea nami. Nami nilikuwa na shughuli nyingi, ninaomba kwa ajili ya zile Muhuri Saba. Ndipo aliniambia kuhusu. . . Imetukia tena, na kurudia tena. Ndugu Roy, kama nikikosea hili, waweza ku—kunitahadharisha. Basi akasema yeye—yeye aliinuka tena, a—asubuhi, nadhani mapema tena, asubuhi. Na hapo aliangalia chumbani akaona Nuru hii kuu, au Wingu juu ya mlima. Akaniuliza, si muda mrefu uliopita, “Je, kulikuwa na kitu fulani kuhusu Wingu likiwa mlimani,” basi nikasema. . . “katika Biblia?”

⁹⁶ Nami nikasema, “Ndiyo, wakati Petro, Yakobo na Yohana walipopelekwa huko juu, na Wingu likamtia uvuli Bwana Yesu. Na—na Mungu akanena, kasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa.” Nilihubiri juu ya hilo hapa, si muda mrefu uliopita. Ujumbe mdogo, ndugu wa kanda wanaweza waelewe, Msikieni Yeye. Nafikiri pengine mnao kwenye kanda. Nina hakika.

⁹⁷ Basi akasema kwamba alipanda juu mlimani. Na alipoupanda, nilikuwa nimesimama pale. Na Sauti ikatoka kwenye lile Wingu, (Sivyo, Ndugu Roy?) Ikasema kitu kama hiki, “Huyu ni mtumishi Wangu. Nami nimemwita kuwa nabii kwa wakati huu, kuwaongoza watu kama tu Musa alivyofanya. Naye amepewa mamlaka, angeweza kunena kitu kiwepo.” Au kitu kama hicho, kama Musa alivyofanya, kama kunena watokee inzi. Nasi tunajua kuhusu wale kindi, na kadhalika, na mambo ambayo tayari yamekwisha kutukia. Maskini Hattie Wright nyuma kule, nadhani mnajua lilotukia kule nyumbani. Na Yeye alimwambia kwamba tayari nimetenda aliyotenda Musa.

⁹⁸ Na sasa yeye aliniambia hivyo, nikishuka kuja baada ya—ya safari. Na bongoni mwangu, nimekwisha amua bongoni mwangu kwamba ningepanda niende kwa Bud, kwa sababu yuko katika hali mbaya juu kule kama mwindaji.

⁹⁹ Kabla ya kuondoka hapa...Naona nitoe neno hili, nasi tutaharakisha. Niliota ndoto ya ajabu, ndoto isiyo ya kawaida. Nami natumaini, shemeji yangu atakapolipata hili, halitamchukiza, na natumaini simuudhi mke wangu, ambaye anaketi hapa sasa. Bali yeye anaijua. Mnamo miezi mingi iliyopita, kuendelea, vema, ilikuwa kama Octoba au Novemba, niliota kwamba ni—nilikuwa ninatangatanga gizani, nami... Vema, si—sikuwa na mahali pa kwenda na hakuna aliyenijali, nami nimekuwa mzururaji, m—mzururaji tu. Nami nilikuwa nasikia baridi, nami nikataza mbali nikaona moto. Nami nilipofika kule, ilikuwa ma—mahali pa kutupia takataka za mji, nao walikuwa na handaki na ule moto ulikuwa kwenye hizi handaki. Basi katikati ya zile handaki, kulikuwa kunateleza, ndiko walilala hao wazururaji, ili wapate joto, wasije wakafa kwa baridi, katikati ya mioto hii, katika usiku wenye baridi kali ya kipupwe. Basi ni—nilikuwa ninasikia baridi. Nami ni—nikaenda hata kwenye moto huu, kupata joto, nao umezungukwa na wazururaji. Nao walikuwa...Sikuona ye yote wao, bali yaonekana kwamba wao walikuwa na vibanda au sehemu ya kulalia. Nami nilimwona shemeji yangu, Fletcher Broy.

¹⁰⁰ Na Fletcher, jinsi nilivyomkumbuka. Ni mtoto mzuri. Bali hili laweza liwe funzo kwa watoto wadogo. Nakumbuka miaka michache iliyopita, kijana mwanamume mzuri, huyu James Fletcher Broy, naye aliungana na kundi baya, naye akanywa pombe kwa mara yake ya kwanza. Namkumbuka akiniita nyuma ya mapazia nyumbani mwangu. Na baba yake amekwenda Utukufuni, miaka mingi iliyopita, alikuwa nje kule akipiga gitaa, “Juu ya kilima cha mbali palisimama msalaba wa kale uparuzao.”

¹⁰¹ Ndipo Fletcher akaniita akasema, “Ndugu Bill, niombe. Sikiliza wimbo huo anaouimba baba yangu, nami nimekuwa nikinywa pombe leo.”

¹⁰² Nikasema, “Fletcher,” mvulana wa umri kama wa miaka kumi na minane, nikasema, “usifuate njia hiyo.” Lakini yeye kamwe hakusikiliza. Aliendelea. Akawa mlevi kupindukia. Ndipo mkewe akamwacha, watoto wake, na yeye saa hii yuko tu... Na Mungu anajua ninampenda.

¹⁰³ Nikaondoka nikaenda kumwomba, mzururaji tu. Nilienda kumwomba, hapa si muda mrefu uliopita, aliumia wakati nilipokuwa hapa kwa ajili ya zile Muhuri Saba. Nilisema, “Fletch, nina suti chache juu kule ninge—ningetaka kukupa.”

Akasema, “Usifanye hivyo, Ndugu Bill.”

Nami na—nalijua hakuwa na nguo. Basi nikasema, “Kwa nini usichukue hizo nguo?”

Akasema, “Ha-aha.” Naye akaniangalia, “unaona, unajua ningezifanyia nini. Nitaziweka rehani nipate kunywa pombe.”

Nami nikasema, “Nitakupa fedha kidogo, Fletch.”

¹⁰⁴ Akasema, “La, usifanye hivyo, Ndugu Bill. Si—si—sitaki ufanye hivyo.” Yeye ni mtu thabiti, moyoni, bali amekuwa mlevi kupindukia na mzururaji. Na mke wa—wake ameshika njia mbaya. Na, loo, karibu kila kitu tu kimpata maskini jamaa yule.

¹⁰⁵ Nami nilipoamka, kabla ya kuamka, Fletch akaniambia, akasema katika ile ndoto, akasema, “Billy nita—nitakutafutia mahali, Ndugu Bill. Uliwalisha watoto wangu walipokuwa na njaa.” Kisha akasema, “Ulikuwa baba kwao. Sasa nitakutafutia mahali hapa upate joto.” Na tulienda tukipita sehemu za wazururaji na hatimaye tukafika mahali fulani, akasema, “Nitaketi hapa.”

Nami nikasema, “Nitaenda juu hapa nione kama ninaweza kupata nafasi.”

¹⁰⁶ Nami nikapanda nikaenda, na kuangalia nje kwenye usiku wenye giza na baridi. Nami nikawaza, “Hebu fikiria jambo hilo. Wakati mmoja, Mungu Mwenyezi ameniruhusu niongoze Kanisa Lake. Wakati mmoja, Yeye aliniruhusu kuhubiri Injili Yake na kuona watu wakiokoka. Wanaume na wanawake wanakuja toka duniani kote, kuzungumza nami kwa dakika chache. Na mimi hapa sasa, mzururaji, na hakuna anayenitaka. Na nina baridi. Basi nifanye nini?” Ndipo nikaamka.

¹⁰⁷ Nilimwambia mke wangu, nikasema, “Labda inamaanisha kwamba Fletch ana haja.” Kwa hiyo tuliharakisha, kuona kama tungeweza kumwona. Na kaka yake akamwona. Alikuwa akikaa nje hapa, pamoja na Weidners. Nje ambako wana...farasi wa biashara na kadhalika; hulala kwenye pembe ya ghala ya chakula au kitu fulani. Nikaendelea. Nikawaza, “Vema, yabidi niliachilie.”

¹⁰⁸ Kwa hiyo nikashuka kurudi sasa kutoka Canada, pamoja na Fred na hao wengine, juzijuzi. Na moyoni mwangu, nilipanga, “Kama watu hawa hawakutaka kusikia Ujumbe wangu, sawa, si lazima wausikilize.” Nilikuwa nimehubiri sasa kwa kama miaka thelathini na mitano. Na miaka kumi na mitano hadi kumi na minane iliyopita sikufanya kitu cho chote ila tu kwa Bwana. Nimejaribu kuishi karibu sana na Yeye na kutosema neno mpaka Yeye ameniambia kwanza, kila kitu.

¹⁰⁹ Watu wanasema, “Naam kama Ndugu Branham akikuambia anakuja, kumbuka, tazamia mkutano huo, kwa sababu anakuja katika Jina la Bwana. Hatafanya cho chote mpaka Bwana aseme...” Hiyo ni sawa. Nilingojea mpaka Yeye akaniambia.

Sikusogea mpaka Yeye aniambie. Na halafu Yeye alipata kuwa, kwa miezi michache iliyopita, Yeye hakuniambia kitu kuhusu mahali nitakapokwenda.

¹¹⁰ Halafu nilishuka kutoka Canada, na Fred akasema . . . Ama Ndugu Roy akanisimulia ndoto yake, huku mimi na yeye na Ndugu Banks tukisafiri pamoja, kabla tu ya sisi kutengana.

¹¹¹ Ndipo basi siku iliyofuatia tulishuka tukaenda kwa Ndugu Fred. Na mwanawe, Lynn, hawakuwepo nyumbani, kwa hiyo hakuweza kuambatana nasi. Yeye na mkewe iliwabidi kungojea. Alimchukua mkewe pale Rosewood . . . au Melrose, Saskatchewan.

¹¹² Basi mimi na Billy tukaja kwa gari la Ndugu Fred. Usiku ule tulisafiri karibu usiku kucha, na siku inayofuatia. Na asubuhi iliyofuata tuliondoka Helena, Montana, na tulikuwa tunakuja kuelekea mpakani.

Nami—nami naweza kukaa mpaka kama saa tatu, kisha nipate usingizi. Yanibidi nilale. Naye Billy, yeye hupenda kulala mpaka kama saa nne siku inayofuata, kukisha pambazuka, kwa hiyo inakuwa, jambo zuri sana kwetu kusafiri.

¹¹³ Kwa hiyo ni—niliamka kwenye saa kumi nikaanza, nikiendesha, naye Billy analala. Tulikwenda mahali fulani nami nilikuwa nikifikiria moyoni mwangu, “Unajua nini? Moja ya siku hizi, mara tu nikiweza kumpeleka mke juu kule . . . Nami sitamwambia nitakachofanya. Lakini ningepanda juu kule, ndipo nitamwambia, Ninapenda sehemu hii sana, hakuna haja ya sisi kwenda mahali pengine. Hebu na tuishi tu hapa.” Na hapo ni huko mbali na ustaarabu, maili elfu moja na mia moja toka po pote pale. Unaona? Huko mbali sana nyikani. Nikawaza, “Jamani, si hilo litakuwa zuri! Haitanilazimu kukatwa nywele, na ha—ha—haitanibidi kuvalia vizuri. Na nitakuwa tu m—mpanda milima wa kawaida, kitu ambacho nimependa kuwa sikuzote.” Nami nikasema, “Nina bunduki chache, na watu fulani walinipa, na nitakuwa kiongozi ambaye hujapata kusikia habari zake. Nitalipenda jambo hilo sana. Ndipo kama Bwana akiniambia nishuke niende nikamwambie mtu fulani jambo fulani, nitachomoka haraka na kuwaambia na kurudi tena. Nami nitamsaidia Bud, nasi tutakuwa kwa kweli na mahali pazuri sana hapa.” Nilikuwa nikifikiri kuhusu jambo hilo.

¹¹⁴ Tulikwenda kwenye mkahawa, kula, mahali padogo mlimani, kwenye saa moja. Majira yalikuwa yameendelea sana, kwa hiyo nilimwamsha Billy. Tuliishiwa na petroli, kwa hiyo ilibidi kununua petroli kidogo. Basi tukaenda kwenye mahali hapa padogo, mkahawa huu mdogo. Na tulipokuwa mle, mtu fulani alikuja akavuka barabara, pengine amenizidi umri kidogo, bali alionekana kama mwanamume, kwangu mimi. Alivaa jozi ya ovaroli, koti la ovaroli, buti za kupandia farasi, kofia nyeusi, masharubu marefu usoni *hivi*, meupe kama theluji,

nywele zake zikining'inia nje tokea chini, nyuma ya kofia yake. Nikawaza, "Huyo anaonekana kama mwanamume, kwangu." Si mtu hafifu, mvivu, na sigara kinywani, ndefu namna *hiyo*, ameketi huku amevaa kaptura, kwenye baraza ya starehe au bwawa la kuogelea, kama mtu fulani wa mashariki mwenye kitambi. Samahani kwa maneno hayo. Bali, hata hivyo, jamaa yule alionekana kama mwanamume, kwangu; mgumu, dume. Alionekana kama aliishi mahali ambapo Mungu alimfanyia mwanaume kuishi. Nami nilikuwa ninampenda.

¹¹⁵ Akaja mkahawani akaagiza keki ya karai. Kulikuwa na kama watu kumi na watano, ishirini. Ilibidi apige chafya. Na unajua jinsi baadhi ya watu wata. . . [Ndugu Branham anaigiza chafya ya kusongwa—Mh.] Samahani. Lakini alipiga chafya kubwa ya mtu mwenye afya, ya mwituni, "At-chii-uu!" Jamani, ilionekana kama madirisha yamepasuka. Alipofanya hilo, hakuna mtu aliyethubutu kusema kitu. La, bwana. Nikasema, "Billy, huyo ndiye mtu anayependendeza moyo wangu."

Akasema, "Aa, baba, hutaki kuwa kama. . ."

"Hivyo ndivyo, huyo ni mimi siku za usoni." Unaona? Nikasema, "Huyo ni mimi."

¹¹⁶ Nami nikaketi pale kidogo, na Billy akanitazama huku anakula keki zake za karai, basi ni—nikamaliza zangu. Mnamo dakika chache, mtu fulani, kibandani papo hapo mbele yetu, na mbao zikiwa upande *huu*, nyuma ya kibanda, sikuweza kuona pande zote. Mtu fulani akasimama, ambaye alifanana kabisa nami, yapata umri wa miaka sabini na mitano, kijitu kidogo. Nguo zake zinambana sana na zimechakaa. Na rafiki aliyeandamana naye alikuwa Fletcher Broy, sawa kabisa, nywele za kijuvujivu zikining'inia usoni mwake. Ndipo Billy akatazama pande zote, akasema, "Baba, huyo anaonekana kama wewe na Fletcher." Unaweza kuwazia jinsi nilivyojisikia. Na maskini kile kijitu, kilichofanana nami, kikayumbayumba. U. . . Walikuwa wamesimama kwenye moto wa kambi, wakiwa na moshi kila mahali, nyuso chafu. Nafikiri kiamshakinywa chao, pamoja, mtu yule lazima alilipa senti ishirini, pengine kikombe cha kahawa au cho chote kile. Moyo wangu ukarukaruka ndani yangu. Nami nikaangalia. Na Billy akasema, "Kuna nini?"

Nikasema, "Hakuna kitu." Nami nikaangalia jambo hilo, nao wakazunguka wakatoka.

Akasema, "Baba, kuna nini?"

Nikasema, "Hakuna." Basi akaingia kwenye gari. Nikasema. . .

Akasema, "Waweza kuendesha tena tafadhali?"

Nikasema, "La."

Akasema, "Bado nina usingizi."

117 Kwa hiyo akaenda kulala, nami nikaendesha kasi barabarani, kama maili hamsini na tano kwa saa, kwenye gari la mizigo, juu ya milima tukielekea m—mpakani, tukishuka kwenda. . . Tukija nyumbani Arizona, lakini nilikuwa nimekaribia sasa Utah. Na nilipofika pale, nikiteremka milimani, yapata maili ishirini toka mjini, kana kwamba. . . Mmelisikia, kama nilivyowaambia kuhusu asubuhi ile kuhusu kindi na mambo yote haya, jinsi kitu fulani. . . Mtu fulani alianza kuzungumza nami, Sauti sawasawa tu na unavyoisikia yangu. Najua inaonekana kichaa. Lakini kama nilivyokwisha kusema, “Je! niliwahi kuwaambia jambo lo lote isipokuwa lililokuwa sahihi?” Na Sa—Sauti ikaanza kuzungumza. Nilikuwa nikizungumza na Yeye.

118 Hiyo ilisema, “Tekeleza mipango yako nawe utakuwa namna hiyo.” Nikasema, “Bwana, sitaki kuwa namna hiyo.”

119 Kasema, “Mkeo atakuacha, pia. Hataishi juu kule kwenye hivyo vilima jinsi hiyo. Na utakuwa mzururaji kama vile ndoto ilivyokuonyesha ungekuwa.”

120 Nikasema, “Sitaki kuwa hivyo, bali ile. . . si—si—sitaki kulazimika kuishi namna hiyo. Na—nataka kufanya tofauti. Lakini mimi ni—niliambiwa kwamba—kwamba Wewe uliniita kuwa na—nabii, nami nataka kuishi nyikani kama wale manabii.” Lakini nilikuwa ninatumia udhuru wangu mwenyewe ili niweze kuwinda; faida yangu.

121 Ndipo Yeye akasema, “Lakini hao walikuwa manabii wa Agano la Kale. Wewe umeitwa kuwepo pale kwenye huduma ya juu zaidi kuliko hiyo.” Akasema, “Una vipawa vingi zaidi kando ya hiyo. Uliitwa kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa na kuhubiri Injili. Na katika namna ya kimitume, unajua kuhusu—kuhusu mambo makubwa zaidi, vipawa vingi vikubwa mno.” Akasema, “Kwa nini unaningojea Mimi nikusukume kila wakati unapotenda kazi? Thawabu yako iko wapi?” Ndipo nikaona. Halafu kasema, “Je, unakumbuka?” Niliwaambia. . . ? . . . “Unakumbuka alilokuambia Ndugu Roberson katika ndoto yako, katika ndoto yake, au ono? Kwamba umefanya kama Musa. Umesahau dhiki ya watu wako. Umesahau mwito ambao nimekuitia.”

122 Niliwaachilia wagonjwa. Nataka Bwana aniambie niende wapi na nisiende wapi. Hilo ni kosa. Nimejitia kinyongo mimi mwenyewe, kwa sababu watu hawakusikia Ujumbe wangu. Na iwapo uta. . . Mungu anizuie nisijaribu kulinganisha maisha ya sasa na ya Musa, bali ni sawa kabisa na alilotenda Musa. Watu wasingemsikiliza alipokuja kuwakomboza, kwa hiyo akawaacha peke yao akaenda nyikani, lakini Mungu alimgeuza. Naye alisahau kitambo mateso ya hao watu.

123 Ndipo basi nikasema, “Bwana, kama. . . Ningewezaje, hilo ni sahihi, bila elimu, kufaulu na elimu ya shule ya msingi?”

Na watu wangesimama kwenye mistari kila mahali, kusikiliza Injili rahisi,” Ni zaidi, ni kubwa zaidi sasa kuliko ilivyokuwa chini ya Agano la Kale. Yeye alipaa Juu na huwapa watu vipawa. Unaona? Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi nilikuwa ninazungumza, nami niliisikia Hiyo ikizungumza nami, Ndipo ikaniacha.

¹²⁴ Nami nikasema, “Billy.” Naye alikuwa amelala fofofu. Nikasema, “Billy, huyo alikuwa ni wewe?” Naye hata hakuamka.

¹²⁵ Nami nikawaza, “Bwana Mungu,” nikapunguza mwendo wa gari langu, “hii inamaanisha nini?”

Na nikasema, “Billy. Billy.”

Kasema, “Unataka nini?”

Basi nikasema, “Ulinizungumzia?”

“La. Kwa nini?”

¹²⁶ Nami nikasema, “Nataka kukuambia jambo fulani. Niliota ndoto si muda mrefu uliopita. Unakumbuka tulipomwona yule mtu aliyefanana nami na Fletcher? Muulize mama utakaporudi Tucson, nilimsimulia ndoto hii. Na, Billy, kuna jambo fulani linalotendeka, linaendelea sasa hivi. Kitu fulani kilikuwa kinazungumza nami, nami—nami nilifikiria ilikuwa ni wewe.”

¹²⁷ Aliniangalia kwa mshangao fulani, na kungojea kidogo, tulikuwa tunaendelea na safari garini. Kwa hiyo, dakika chache, akalala tena. Nami nilikuwa ninaendesha, nikiwazia jambo hilo linamaanisha nini? Nikiendesha gari, barabarani kabisa, na, mara, Hii hapa inakuja ikizungumza tena.

¹²⁸ Naye akasema, “Rudi! Hivi sikukuambia wewe, mwanzoni, kufanya kazi ya mwinjilisti? Nilipokuita kule chini mtoni, hivi sikusema, ‘Kama Yohana Mbatizaji alivyopelekwa kutangulia kuja kwa kwanza?’ Yohana hakuwa zaidi ya nabii? Yesu alise’Mlitoka, Yeye Mwenyewe. ‘Mlitoka kwenda kuona nini, nabii?’ Kasema, ‘Zaidi ya nabii.’”

¹²⁹ Halafu yote ikaanza kunielea. Nikaanza ku—kushangaa. Halafu akanikumbusha tena kuhusu wale—kuhusu wale watu. Jinsi, kufanya ambalo Musa alifanya, Musa angeweza kuwafikia watu akiwa nyikani? Nami ningeweza kuwafikia watu nikiwa nyikani? Jambo lile lile hasa. Halafu ikafikia kwenye hili, Timotheo wa Pili 4. Kumbuka tulipoweka wakfu kanisa asubuhi ile, miaka thelathini iliyopita, baadhi yenu ninyi watu wa siku nyingi, wakati Yeye aliponionyesha mimi hiyo miti nami nikaipanda pande zote mbili? Mnakumbuka hilo? Mnakumbuka ono hilo. Yote yameandikwa katika vitabu na katika kanda na kila kitu. Imekuwa miaka mingi iliyopita, jinsi nilivyoona haya na—na kamwe sijajiunga na Umoja au Utatu. Nimesimama katikati yao na kupanda miti hii, na ndiyo miti miwili pekee iliyokuwa na matunda. Nami . . . Miti yote ilikua

hadi kama futi thelathini kisha ikakoma. Hii ilikwenda moja kwa moja hadi Mbinguni; imekatwa toka kwenye tawi lile lile. Unaona? Mmoja upande mmoja na mwingine upande mwingine, nami niliivunja. Mnakumbuka lile ono. Unaona? Limeandikwa kwenye vitabu na limo katika simulizi la maisha yangu na kadhalika. Nayo ilikwenda hadi Mbinguni hivyo, haraka. Kisha akasema, “Nyosha mikono yako uchume tunda.” Ndipo nilikuta tunda lile lile msalabani, nilipokimbil’Fanya. Kisha akasema, “Fanya kazi ya mhubiri wa Injili. Timiza huduma yako. Na wakati utakuja watakapoyakataa mafundisho yenye uzima.’ Usiwaache basi. Endelea.” Hayo yote yakanielea moyoni.

¹³⁰ Ndipo namkumbuka huyu Marilyn Monroe, msichana ambaye nilimwona akifa yapata juma moja kabla hajafa, na jinsi ambavyo wao walisema alijiua, ambapo hakujiua. Niliwaambia kuhusu jambo hilo, hapo awali, ambalo lingetukia, na lilitukia. Na kama ilivyotukia kwa wale mabondia juu kule; mmoja alikuwa anaenda kumuua mwingine. Sikumfahamu vyema yule msichana. Kuna msichana mwingine pale, mpwawe ni—ni—ni Danny Henry. Anaitwa nani? Jane Russell. Mpwake, mvulana wa Kibatisti.

¹³¹ Nami nilikuwa nikihubiri huko Los Angeles, kwenye kiamshakinywa cha Wafanyi Biashara. Basi nimesimama pale nikiyakemea yale madhehebu, na hapo aliketi mkuu wa Waassemblies, na wengi wa viongozi waheshimiwa wamekusanyika pale. Nami nilipomaliza kuzungumza na nikaanza kuondoka jukwaani, nikijitayarisha. . . Sababu, Ujumbe huo ulikuwa unatangazwa nchini ko—ko—kote, kwa redio, basi, na ilibidi ibadilishe. Katika badilisho hili, walipofunga redio, basi, ili kuutangaza Ujumbe ule, na kurudi na kutangaza stesheni. Nami nilikuwa huko Clifton, ambako tuna kiamshakinywa. Basi nilipokuwa ninatembea kutoka kwenye jukwaa la juu hadi la chini, kijana mvulana mwenye sura nzuri na mwenye umri wa kama miaka thalathini, akatoka mbio akanikumbatia. Akasema, “Mimi ni Danny Henry.” Nami sikujua kwamba huyo anayeshughulikia televisheni ni kaka yake. Nayo hiyo televisheni huwashughulikia hao Wakristo Wafanya Biashara. Na Jane Russell, yule mchezaji mashuhuri wa sinema, mpwake. Mama yake ni mhubiri wa Kipentekoste.

¹³² Na basi alipoanza kunikimbilia, kisha akanikumbatia, akasema, “Mungu akubariki, Ndugu Branham.” Akasema, “Natumaini hili halisikiki kama kukufuru, bali, nionavyo mimi, huo Ujumbe ungeweza kuwa sura ya 23 ya Ufunuo.” Naye aliposema hivyo, akaanza kunena kwa lugha. Mvulana ambaye hajawahi kamwe kusikia jambo kama hilo, ni wa madhehebu ya Kibatisti. Na mara. . . Aligeuka akawa mweupe, naye akaniangalia. Hakujua la kufanya. Kuna watu waketi hapa waliokuwepo pale. Ulikuwepo pale, Fred? Ni wangapi

walikuwepo pale wakati ule? Ndiyo, kuna hao watatu hapa, waliokuwepo pale wakati ule. Naye hakujua la kusema.

¹³³ Na hapo palikuwepo na mwanamke mnene mno wa Kifaransa ameketi chini hapa. Akainuka, akasema, “Mbona, hilo halihitaji kufasiriwa kamwe. Hicho kilikuwa Kifaransa kitupu.”

Huyo mvulana akasema, “Sijui hata neno moja la Kifaransa.” Basi mwanamke yule alikuwa ameandika aliyosema.

¹³⁴ Halafu palikuwepo na mwanamume amesimama pembeni, akasema, “Hilo ni sahihi. Nimeandika aliyosema, ni Kifaransa.” Huko nyuma kabisa, jamaa mzuri mwenye nywele nyeupe ya shaba, aliyesimama kugemea ukutani, alitokeza na kulinganisha hayo maandishi. Yeye alikuwa mkalimani wa Kifaransa katika Umoja wa Mataifa. Na mtu huyu hapa alikuwa Victor LaDeaux, wa kanisa la Arne Vick nje huko, naye akayaandika. Nami nina tafsiri yake.

¹³⁵ Sikilizeni haya, kama ninaweza kuyasoma.

Mimi, Victor LaDeaux, ni Mfaransa kamili asiyechanganywa damu; Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, aliyejazwa Roho Mtakatifu. Anwani yangu ni 809 North King Road, Los Angeles 46. Ninahudhuria Hekalu la Bethel, Mchungaji Arne Vick, mchungaji. Tafsiri ya kweli ambayo ninatangaza, ya unabii uliotolewa juu ya Ndugu Branham, ukatolewa na Danny Henry katika Kifaransa, Februari 11, 1961, kwenye kiamshakinywa cha Wakristo Wafanyi Biashara wa Injili Yote. Tafsiri ya kweli ya huo unabii.

¹³⁶ Sasa hivi ndivyo Hiyo ilivyosema:

Kwa sababu wewe umechagua njia iliyo nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi, wewe umeenenda kwa chaguo lako mwenyewe. (Sasa, naweza kuona hilo. Ilimbidi Musa kujichagulia, pia. Unaona?)

Wewe umechukua njia iliyo sawasawa na sahihi, uamuzi sahihi, nayo ndiyo NJIA YANGU. (Imepigiwa mstari, “NJIA YANGU,” Roho Mtakatifu akijibu.)

Kwa sababu ya uamuzi huu ulio muhimu sana, sehemu kubwa ya Mbingu inakungojea . . . inakungojea wewe.

Ni uamuzi mzuri jinsi gani . . . (Sasa sikiliza kwa makini) . . . Ni uamuzi mzuri jinsi gani umefanya. Jambo hili lenyewe ndilo lile ambalo litafanya, na kutimiza, ule ushindi mkuu katika upendo wa Kiungu.

¹³⁷ Unaona, ni kitendo kabla ya kielezi. Unaona, Kifaransa. Sasa mkalimani wa Umoja wa Mataifa alifasiri hayo. Na yule mvulana hajui hata neno moja, hajasikia kamwe—hajasikia kamwe kitu kama kunena kwa lugha. Yeye alikuwa

Mbatisti. Alikuwa huko tu bila kutazamia, aliposikia huo muziki ukichezwa, ndipo akaja pale na kusimama pale na kunisikiliza nikihubiri.

¹³⁸ Sasa, “katika upendo wa Kiungu,” upendo wa Kiungu. Huo wawezaje kuwa upendo wa Kiungu kama si Ro—Roho Mtakatifu? Roho Mtakatifu ndiye upendo wa Kiungu.

¹³⁹ Naam, na wakati mimi na Billy tulipoanza kwenda barabarani, unaona, tulipoanza kwenda zetu barabarani, Billy aliingia usingizini tena. Na Hiyo ikasema, “Nitakupa wewe ishara ya milele.”

¹⁴⁰ Nami nikasema, “Bwana, ipi . . .” Nilingojea kidogo na hakuna lililotukia. Nikasema, “Ishara ya milele ni ipi, Bwana?” Ndipo nikangojea dakika chache. Mara nikageuka kumtazama Billy; alikuwa amelala.

¹⁴¹ Kisha akasema, “Nitakupa ishara ya milele,” tena. Akasema, “Tazama upande wa magharibi kutoka ulipo.”

¹⁴² Basi nikageuza kichwa changu hivi katika gari la mizigo, kutazama; nikapunguza mwendo, halisi. Ndipo, loo, jamani, Roho wa Bwana! Nilijisikia kama ningeweza kupiga mayowe na kulia. Basi nilitazama, nikaangalia, nikaona tu mlima ulio na vilele vyenye theluji juu yake. Nikasema, “Sijui, sioni ishara ya milele kuhusu hilo.”

¹⁴³ Yeye akasema, “Jina lako limeandikwa kila mahali juu yake.”

¹⁴⁴ Loo, nikawaza, “Hilo ni jambo gani?” Nami nikawa mnyonge kweli na nikaanza kusimama.

¹⁴⁵ Na Billy akaamka akasema, “Una nini?” Nami nilikuwa nimeweka mikono yangu *hivi*, jasho likidondoka katika mikono yangu, na theluji inaanguka.

¹⁴⁶ Nikasema, “Billy, kitu fulani kinatendeka. Wakati mmoja najua ambapo nilipokosea. Najua kwamba nimemkosea Mungu.” Na ilionekana kama ningeweza kusikia wimbo ule ukiimbwa, na kuona maelfu ya watu waliochanganyika, viwete, vilema, vipofu, na waliopooza; nikasikia kwaya, sauti ya mtu maarufu sana, ikiimba:

Mchafu! Mchafu! Pepo wachafu walimpagaa.

(Mnajua ule wimbo.)

Ndipo Yesu akaja na kuwaweka wafungwa huru.

¹⁴⁷ Niliweza kuona mistari ya wagonjwa ikitandaa kila mahali, ikanibidi kusimama. Billy hakujua nini kilichokuwa kinatendeka. Na nikatazama juu.

¹⁴⁸ Nikasimama nikatazama juu ya ule mlima, nami nikaona vile vilima saba. Naam, hapa, iwapo unataka kuona jambo fulani. Kulikuwa na vilele saba juu ya mlima, mlima mmoja,

ulitandaa kwa maili nyingi. Mlima wa mwisho kabla ya kuingia katika nchi nyingine; hakuna milima mingine baada ya huo. Na ulikuwa ukitandaa kutoka mashariki hadi magharibi, mgongo wa mlima, na kilele chake kimefunikwa na theluji.

149 Vilele viwili vya kwanza, halafu kilele kikubwa; halafu kilele kingine kidogo, na halafu kilele kikubwa zaidi, na halafu kilele kidogo, na halafu mlima mkubwa mno, na mpana, uliofunikwa na theluji. Nami nikasema, “Bwana, sielewi maana yake.”

150 Yeye akasema, “Kuna vilele vingapi?”

151 Nikasema, “Kuna saba.”

152 “Jina lako lina herufi ngapi?” B-r-a-n-h-a-m, M-a-r-r-i-o-n B-r-a-n-h-a-m.

153 Na kulikuwa na vilele vitatu vilivyojitokeza. Yeye akasema, “Vilele hivyo vitatu ni ule mvuto wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Wa kwanza ulikuwa sehemu yako ya kwanza ya huduma, kilima kidogo, halafu mvuto wako wa kwanza, kirefu sana.” Mnajua, ishara mkononi. Halafu kulikuwa na kipindi kidogo hapo, muda ule nilioondolewa kwa kuchoka mno. Wengi wenu mnakumbuka jambo hilo. Ndipo ukaja ule upambanuzi, mvuto wa pili. Sasa nimekuwa na kingine, mnamo miaka michache hapa ya namna fulani ya vilele vidogo tu, kurudi nyuma kana kwamba huduma yangu haijaanza bado, na halafu ukaja ule wa tatu.

154 Tatu ni nambari ya kumaliza, mnaona, wa tatu. Kilele kinachofuatia kilikuwa cha tano, namabari ya neema. Na kilele kinachofuatia kilikuwa cha saba, nambari ya—ya ukamilifu, mwisho. “Siku sita fanya kazi. Ya saba ni Sabato,” mwisho wa juma, mwisho wa wakati. Mnaona? Nami nikasimama na kumwonyesha Billy jambo hilo. Na nikaangalia jambo hilo.

155 Yeye kasema, “Basi na iwe hivyo. Iwapo kuna shaka wakati wowote moyoni mwako, kumbuka mahali hapa, rudi mahali hapa.”

156 Na Billy akanipiga konde begani, akasema, “Baba, angalia mashariki!” Na jinsi lilivyotukia, sijui, bali huko upande wa mashariki wa ile barabara kulikuwa na lundo lile la uchafu linaloungua. Maili na maili kutoka aina yo yote ya mji, tita la takataka za kale likiwa hapo upande wa kushoto wa barabara.

157 Ninarejea kazini. Amina. Mzee au kijana, niishi nife, nitamtii Mungu mpaka mauti yatakaponiweka huru. Nimemkosea Bwana, si kwa kukusudia. Au ninafanya... Nimejaribu... Hebu niingize hili. Unaona? Kanda imebakia? Hebu niingize hili. Nimetamani, nimetamani kumwona Yesu Kristo akidhihirishwa bila ya waa hata moja. Basi hebu ndugu wanaosikia kanda hii, na kanisa hili likimbuke, tangu leo, sababu ya ninyi kutokupata waa, na sababu ambayo ninyi kwa miaka hii yote hamwezi kusema hata jambo moja lilitukia kunenwa au kutendwa isipokuwa ambalo lilitokea.

Namhimiza mtu ye yote alete jambo lo lote katika maelfu ya yale mambo humu jukwaani, na upambanuzi, na ubashiri wa yale yangetukia; yametukia barabara kabisa. Naam, iwapo kanisa linaamini hilo, liseme, “amina,” ili kwamba... [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakuna hata mtu mmoja ulimwenguni awezaye kuonyesha jambo moja. Lakini na ijulikane kwa kanisa hapa na kwa kanisa la baadaye: kama Mungu akimsukuma mtu ampitishe katika bomba, na hasogei kamwe mpaka Mungu amwambie, hamna imani katika jambo hilo. Ni Mungu akikusukumiza kwenye jambo fulani. Na limejenga huduma hii hadi kufikia mahali ambapo hakuna mtu ye yote awezaye kunena neno moja dhidi yake. Bali tangu sasa, hebu kwanza ninene nanyi katika Jina la Bwana, kabla ya ninyi kusikiliza, kwa sababu yanibidi niondoke niende kwa imani. Lazima nilitende kwa imani, au ninafikiria ni sawa au si sawa, au cho chote kile. Ninatenda nionavyo mimi ni bora, kisha naondoka kulitenda. Sababu ya kutokuwa na kosa, ni kwa sababu nimengojea mpaka Yeye aniambie niende nikalitende. Nimemngojea Yeye. Kwa hiyo haikuwa ni mimi; ilikuwa ni Yeye.

¹⁵⁸ Lakini, mnaona, hata yule Mtakatifu Paulo maarufu aliingia mashakani wakati mmoja. Na mara nyingi ambapo Mungu amefanya mambo au ameachilia watumishi Wake wayafanye, yalitokea makosa, ili kuthibitisha mambo haya. Naam, tunajua kwamba binadamu anaweza kufanya makosa, bali Mungu hawezi akafanya kosa lo lote. Bali sasa kama nikiingia kwenye uwanja wa kuhubiri, na kuenenda jinsi ni—ninavyoenenda, basi inanibidi nipange mikutano kabla na—na kuweka mambo sawasawa. Na labda huu ndio ule wakati mkuu unaokuja ambao tumekuwa tukiutazamia. Na hakika iwapo “Jambo hili lenyewe ndilo jambo kuu ambalo litatimiza, na kufanya utimie, ule ushindi mkuu katika upendo wa Kiungu,” na hicho ni kitendo kabla ya kielezi, basi ni upendo wa Kiungu, ambao ni Mungu. Unaona? Na inahitaji upendo wa Mungu kukimbilia kwa haraka nje kule kwenye mstari wa mbele na kusimama katika pengo kwa ajili ya watu.

¹⁵⁹ Na hawa akina Ricky na Ricketta ambao nimewakemea sana kwa Maneno, na nimewaita “Ricky” na “Ricketta,” Mungu amenipa kufahamu hainipasi kufanya hivyo, kwa sababu wengi wao bado ni watoto Wake. Mimi ni... Hawawezi kujizuia kwa sababu wanatenda tofauti kabisa. Baadhi ya haya makanisa mazee na ya kidesturi yanayo roho ile juu yao, nao wame—wamefungwa kama Israeli walivyokuwa kifungoni, vile vile kama Musa alivyokwenda kuwakomboza kutoka utumwani. Binadamu ambao walimpenda Yesu Kristo, wangelintumikia Yeye kama tu wanajua cha kumtumikia nacho. Nao wako kifungoni chini ya umadhehebu unaowaambia, “Msitende *hili*, na msitende *lile*.”

¹⁶⁰ Lakini mwito wa Mungu lazima uje, “Ye yote atakaye kwenda kwenye Nchi ya ahadi, na atembe.” Tunaenda zetu kwenye Nchi ya ahadi. Amina. Hebu na waje, watembe. Tumo njiani kwenda kumlaki Kristo wakati wa mwisho. Nami nilitaka kuleta jambo hili kwenu mpate kuona, na kuwaonyesha hilo, kosa ambalo mtu anaweza kufanya, na hata hivyo ana moyo safi.

¹⁶¹ Musa aliacha kujali dhiki za watu wake kwa sababu wasingemsikiliza. Basi, Ndugu Roy, unaona ndoto yako? Na sasa siwezi kuendelea, na huduma kama hiyo, mpaka nijisikie tofauti moyoni mwangu kuhusu jambo hilo, haidhuru kama Mungu aliniambia. Bali hilo ndilo lile badiliko Ndugu Roy... ambalo uliona likija. Yabidi jambo fulani linibadilishe, kwa sababu mimi, moyoni mwangu, kama nikitoka nje huko nikijisikia namna ninavyojisikia sasa, bado najisikia kwamba wanapaswa kuwa wamesikia Ujumbe ule, wangepaswa kufanya hivyo. Na sijali dhiki za watu inipasavyo. Mpaka nipate kujisikia huko, hakuna haja ya mimi kwenda, kwa sababu ningekuwa mnafiki.

¹⁶² Na miaka yote hii nimejaribu kumtumikia Yeye kwa uaminifu, nami sitatoka kwenda nje huko nikiwa mnafiki. Yanipasa kusikia hivyo, kwamba si *Ricky* na *Ricketta*, na si kundi hili. Ni watoto wa Mungu walioko utumwani, nami yanibidi niwaendee. Mpaka niweze kujisikia namna hiyo, itanibidi tu kuzururazurura hapa na pale, nihubiri katika mikutano fulani na mambo mbalimbali, lakini ningojee.

¹⁶³ Ninao wimbo mdogo. Siwezi kuimba. Ningetaka tu kuunukuu kwenu. Ndugu zanguni, nilivandika tu kwa namna fulani. Bado sijaujaza. Haujaandikwa sawasawa. Sijui kama ninaweza hata kuusoma au la. Uko katika tuni ya *Wimbo Wa Vita Vya Jamhuri*, “Utukufu! utukufu, haleluya!” Mmeusikia. “Utukufu! utukufu, haleluya!” Ni wangapi? Bila shaka, sote tumeusikia huo.

Mhubiri wa mzunguko alizunguka nchini huku
amepanda farasi,
Akiwa na bunduki begani mwake na Biblia
mkononi mwake;
Aliwasimulia watu wa mbugani habari za Nchi
ya ahadi na ya heri,
Alipokuwa amepanda farasi, huku anaimba.

Kuegemea, kuegemea,
Kuegemea kwenye mkono wa milele;
Kuegemea, kuegemea,
Kuegemea kwenye mkono wa milele.

Alihubiri kuja kwa hukumu ya moto na
kiberiti;
Na Mbingu za raha zisizo na mwisho za
waliohesabiwa haki pekee.

Alipopanda kuvuka milima ungeweza
kumsikia akiimba wimbo huu,
Aliposafiri amepanda farasi.

Imo nguvu, nguvu, nguvu ya ajabu
Damuni mwa Yesu
Imo nguvu, nguvu, loo, nguvu ya ajabu,
Msalabani mwa Yesu.

164 Mhubiri mzee wa mzunguko. Mnamkumbuka. Unaona?

Sasa bunduki yake imechakaa na ina kutu, na
inaning'inia ukutani;
Biblia yake imechakaa sana na ina vumbi,
na ile . . . haijaguswa hata kidogo kwa nadra,
(hilo ni kweli)
Bali Ujumbe ambao Hiyo inatuletea sisi
utakutana nasi siku ile,
Kwani Ukweli wa Mungu bado unasonga
mbele.

Wote:

Utukufu! utukufu, haleluya!
Utukufu! utukufu, haleluya!
Utukufu! utukufu, haleluya!
Ukweli Wake unasonga mbele.

165 Nitajifunza huo. Nilisema asubuhi hii nilipokuwa
ninauandika huo, nikaweka mkono wangu juu ya bunduki yangu
iliyochakaa inayoning'inia ukutani. Nikawaza, "Haitachukua
muda mrefu."

Bunduki yake imechakaa na ina kutu, huku
ikining'inia ukutani, (hilo ni kweli)
Na Biblia imechakaa na ina vumbi, na
haijaguswa kwa nadra hata kidogo;
Bali Ujumbe wake toka kwenye biblia hii . . .
siku ya Hukumu siku moja;
Na Ukweli Wake unazidi kusonga mbele.

166 Ukweli wa Mungu katika Biblia hii! Ndiyo. Yesu Kristo ni
yeye yule, jana, leo, na hata milele.

167 Mhubiri mzee wa mzunguko mwenye bunduki mgongoni
mwake, Biblia yake mkononi, alipanda farasi mbugani na
kupanda milima, na kushuka kwenye mitaro na kila mahali,
akihubiri Utawala ujao wa Miaka Elfu, kuhusu Hukumu ya moto
ijayo kwa wasio haki, na kuhubiri Ufalme wa Mungu kwa wenye
haki. Ni kweli. Winchester ya kale inashika kutu. Na Biblia,
wao-wana vitabu vya uzinzi badala ya Hiyo. Lakini Ukweli wa
Mungu bado unasonga mbele. Hujifanya Mwenyewe dhahiri vile
vile leo, na hulithibitisha, kama Yeye alivyowahi kuwa. "Ukweli
wa Mungu unaendelea mbele!"

Utukufu! utukufu, haleluya!
 Utukufu! utukufu, haleluya!
 Utukufu! utukufu, haleluya!
 Ukweli Wake unasonga mbele.

¹⁶⁸ Kwa nini? Mtu fulani atauchukua Huo. Kwa kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hebu na tuuimbe tena. Sasa tumechanganyikana hapa, Mmethodisti, Mbatisti, Mluteri, na kadhalika. Wakati tunaimba pambio hilo la mwisho, hebu tupeane mikono na mtu fulani aliye karibu yako, kisha tutaruhusiwa kufumukana.

¹⁶⁹ Na sasa, kumbuka, wewe ambaye itakubidi uhudhurie kanisa lako mwenyewe, nenda mle usiku wa leo. Mpe mchungaji salamu zangu. Na—na halafu mniombee, kila mmoja wenu. Na halafu tena nataka ukumbuke, kama huna mahali pa kwenda . . . [Ndugu Branham anamwambia Ndugu Neville, “Na kama ungekuwa na cho chote.”—Mh.] Baada ya ujumbe wa Ndugu Neville usiku wa leo, baada ya kumaliza ujumbe wake, basi nataka kunasa kanda inayoitwa *Kimulimuli Chekundu Cha Kuja Kwake*, unaona, usiku wa leo. Bwana awabariki sasa. Na juma lijalo, mimi, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, naweza nishuke tena nije kunasa kanda nyingine, sababu itanibidi kuweko Arkansas juma hili lijalo.

¹⁷⁰ Sawa, sasa hebu na tuimbe tena, na tupeane mikono sasa.

Utukufu! utukufu, haleluya!
 Utukufu! utukufu, haleluya!

Bwana Yesu, bariki lesu hizi! . . . ? . . . [Ndugu Branham anaomba wakati mkutano unaimba—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, tunaweka mikono juu ya lesu hizi.

. . . juu yake.

Mungu atukuzwe! Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

¹⁷¹ Umewahi, Ndugu Ruddell. Hebu njoo huku kidogo uombe. Ndugu Ruddell, mwingine wa ndugu zetu washiriki hapa, wa makanisa madogo yanayoshirikiana pamoja, muungano wa makanisa mbalimbali. Nami nimesikia msimamo wa kishujaa ambao Ndugu Ruddell amechukua kwa ajili ya—kwa ajili ya Injili. Na kwa hiyo na—nasema hivi, Ndugu Ruddell, kwamba kila kitu njiani. . . Mungu hakuahidi kitanda rahisi cha maua. Bali Yeye aliahidi vita, ndiyo, bali aliahidi ushindi. Jambo ndilo hilo.

¹⁷² Nakumbuka mara ya kwanza nilipochukua msimamo huu, hata mama yangu na baba yangu walitaka kunifukuza nyumbani. Unaona? Bali, loo, jamani, jinsi nilivyowabatiza katika Jina la Bwana Yesu! Matumaini pekee niliyowahi kuwa nayo leo ni kwa sababu ya msimamo huo. Nina furahi sana kwamba Ujumbe wa Biblia, tangu yule mhubiri mzee wa

mzunguko hadi wakati huu... Ingawa watu wameushika Huo na wameupamba kila mahali, na wameunda madhehebu na kuweka kanuni za imani na kila kitu ndani Yake, Kweli hiyo bado inasonga mbele. Hiyo ni kweli. Bado inasonga mbele.

¹⁷³ Mungu awabariki, kila mmoja, nasi twatumaini kuwaoneni tena hivi karibuni. Hadi wakati huo, mwaweza kunifanyia fadhili hii moja sasa, ninyi mlio hapa na ninyi mnaosikiza kanda pia, enyi ndugu zanguni? Ombeni kwamba Mungu ataweka moyoni mwangu kile kitu nilichopoteza nje huko katika kile kinyongo. Ni rahisi sana kupata kinyongo.

Nilikuwa na maongezi juzijuzi na Ndugu yangu Way anayeketi hapa, amesimama hapa mbele. Mtu mzuri, bali amejipa kinyongo, aina nyingine ya kinyongo, alitenda jambo lile lile. Ndugu Way, unaweza kulitenda kwa urahisi sana; ni wewe tu ukiingiza kitu kidogo bongoni mwako, unaendelea kuwazia namna hiyo. Rudi ulitazame katika Maandiko, uone au ni sawa au la, ndipo uendeleo tokea hapo. Ndiyo. Usiache kujali dhiki ya watu. Unoana? Yakubidi ukumbuke hawakufanyizwa kwa unga wa mbao. Wao ni nyama na damu, wanadamu wenye nafsi. Niombeeni, ninyi nyote, tafadhalini. Mungu awabariki sasa.

Tutainamisha vichwa vyetu na kumsihi ndugu Ruddell kama ata...

¹⁷⁴ Samahani? [Ndugu Parnell anasema, “Ndugu Branham, nina jambo fulani ningetaka kusema, itanichukua nusu sekunde tu.”—Mh.] Sawa, ndugu. [Ndugu Parnell anasimulia ndoto aliyoota.] Mungu asifiwe! Huyu ni mhudumu. Mtu anaweza asijue. Naye alikuwa mmoja wa kundi lile ambalo, sikupata wakati asubuhi hii, ambaye alikuwa katika moja ya zile ndoto, akizungumzia kuhusu mimi kupitia njia ile nyingine, unaona, kwenda Magharibi, kwenda upande wa Magharibi katika wakati huu wa mwisho. Ndugu J.T. Parnell.

¹⁷⁵ Sasa, kunaweza kuwe na wageni ambao wanashangaa kuhusu watu kupata ndoto, kuhusu waotaji. La, hatufuati aina zote za ndoto na kadhalika, bali sisi tunaamini kwamba Biblia ilisema, “Itakuwa katika siku za mwisho, kwamba nitaimwaga Roho yangu juu ya watu; nao watatabiri, na wataona maono, na kuota ndoto.” Na maadamu hilo liko ndani ya Biblia, ni wajibu wangu kuliamini na kulihubiri. Na watu wanaposimulia ndoto, kama Bwana hataifasiri, tunaiachilia. Na iwapo ni kitu fulani... Wakati mtu ye yote anaponena kwa lugha, lazima liwe jambo fulani kwa kanisa, na lazima hilo nalo litukie, pia. Sisi hatuzifuati, ingekuwa pepo mchafu. Lazima itimie, sababu tafsiri ya lugha ni unabii. Tunajua hiyo ni kweli. Kwa hiyo tunajaribu hapa kuishi Biblia namna ile tu Hiyo inavyofundishwa. Usiondoe lo lote Kwayo au usiongeze lo lote Kwayo, bali hebu uishi Hiyo jinsi ilivyo. Bwana na abarikiwe. Hiyo ilinisaidia, Ndugu J.T., kuamini jambo hilo... Mungu

hakuniambia niondoke niende nikapatane na dhambi; bali niondoke niende na kuendelea kufanya kazi. Unaona?

¹⁷⁶ Hebu tuombe sasa. Ndugu. . . [Dada fulani katika mkutano anapiga mayowe—Mh.] . . . Mtu fulani amezimia. Hebu kidogo. Kaeni kimya, kila mtu. Unaona? [Ndugu Branham anaondoka mimbarani na anashuka kwenda katika kusanyiko.]

¹⁷⁷ Baba wa Mbinguni, hebu rehema Yako na wema vije vikutane na Ndugu Way. Katika Jina la Yesu Kristo, hebu na arudi. Mrudishe, Bwana, na umpe nguvu na afya.

Hivyo anisadie, moyo wake unaanza kupiga tena! Tulieni, kila mmoja, na muombe tu.

Bwana Yesu, jalia wema Wako na rehema Yako viwe pamoja na Ndugu Way, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁷⁸ Imekwisha. Nikisimama hapa kwenye madhabahu haya, ambapo mazishi yamehubiriwa. Mahali ninaposimama hapa, ambapo mamia ya watu wamemsihi Kristo kabisa. Nilimfikia, macho yake yamegeuka, mapigo ya moyo wake yamekoma. Mara nilipoliita Jina la Yesu Kristo, mapigo ya moyo wake yakaanza kurudi tena. Bwana asifiwe! Bwana asifiwe! Kama mtumishi wa msalaba, ninasema hilo katika Jina la Yesu Kristo. Je, Yeye si wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ugonjwa wa moyo. Unaona? Ninashukuru mno umetukia sasa hivi, badala ya kungojea mpaka tumeondoka. Unaona neema ya Mungu? Bwana na abarikiwe!

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁷⁹ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe sasa kwa wema Wako na rehema Yako. Wakati wote Wewe uko katikati yetu. Nipe, Bwana, Mafuta katika taa yangu. Nipe ile—ile—ile Fimbo ya Bwana, ili niweze kuinyoosha Hiyo, juu ya wagonjwa na wanaoteseka. Ili niweze kuleta kwetu juu. . . Kuwaletea ukombozi wanaouhitaji, na hukumu kwa wale wanaoukataa. Tujalie, Baba. Tunakushukuru Wewe kwa wema Wako wote, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ndugu Ruddell, Mungu akubariki ndugu.



KUSIMAMA KATIKA PENGO SWA63-0623M
(Standing In The Gap)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Juni 23, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org